

MBONA UNALIALIA? NENA!

 Hebu tuendeleo kusimama kwa muda mchache, tunapoinamisha vichwa vyetu. Kuna haja maalum? Ukiweza, hebu ijulikane unapomwinulia Mungu mikono yako, na kusema kwa hiyo, “Bwana, unajua haja yangu.”

Baba uliye Mbinguni, sisi ni watu tulioheshimika kabisa asubuhi hii kukutanika katika nyumba ya Mungu, tunapojua ya kwamba kuna watu wengi sana ambao wangetaka kuwa katika nyumba ya Mungu asubuhi ya leo na wamo hospitalini na vitandani mwa magonjwa, nawe umetupa heshima hii kuwa nje leo. Nasi hatuji kamwe, Bwana, kuonana mmoja kwa mwingine, ingawa tunapenda ushirika wa sisi kwa sisi, bali tungalifanya hivyo manyumbani mwetu; bali tumekuja hapa kushirikiana na Yeye Yule ametuunganisha pamoja kama watoto wapendwa na wandugu.

Tunakushukuru sasa. Na njia pekee tujuayo kushiriki vyema na Wewe ni kwa Neno Lako; Neno Lako ni Kweli. Tumekusanyika hapa kwa ajili ya nguvu za kiroho; tunazihitaji, Bwana. Hatuna budi kuwa na nguvu kustahimili misalaba tunayobeba. Tunaomba kwamba utamtuma Roho Mtakatifu aliye mkuu leo, naye atatupa nguvu sisi sote. Tujalie mahitaji ya watu Wako wanapokutanika na kuinua mikono yao Kwako ya kwamba wanahitaji mambo kama hayo. Jibu kila mmoja, Bwana.

Tunakushukuru kwa kuyahifadhi maisha ya Dada Ungren usiku uliopita katika ajali ya barabara humu. Ulikuwa wa rehema, kwao, Bwana, na tunakushukuru kwa sababu ya hayo.

Na sasa, tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi, na kutusaidia tunaposafiri—kila mmoja wetu. Tupe nguvu Zako za kujikinga katika imani ya kujua ya kwamba uwepo Wako usioshindwa utakuwa pamoja nasi. Hiiyo saa ambapo hatuwezi kujisaidia, tunajua Malaika za Bwana wamefanya kituo wakiwazunguka wamchao, nao watatuchukua ili wakati wote tusije tukajikwaa miguu yetu katika jiwe. Tunaomba ya kwamba utatupa baraka Zako kwa ajili ya Neno, na kunena kupitia kwetu—ndani yetu, katika Jina la Yesu. Kristo Amina.

Ninashukuru ya kwamba nuru ya jua la nje, jua la sayari, linaangaza. Kulikuwa kubaya sana asubuhi ya leo, nami nafikiri katika nchi hii hasa, tuna utusitusi mwingi, hali ya hewa inayochosha; na kuona jua likiangaza, likichomoza, ni vizuri sana.

Ule muungano wa jamaa leo—nalikutana na ndugu zangu katika nyumba ya dada yangu na jamaa zetu kutoka pande

zote mjini na vitongoji vyake... Kundi kubwa la Wabranham, kama wanalikutanika kutoka Kentucky, na hapa, nakisia ingetulazimu kukodisha mji mzima; ni wengi sana. Lakini kulikuwa kurudi nyumbani kudogo... Tulizoea kukutana kwa Mama naye alikuwa kama kizingiti kinachotuunganisha. Bali Mungu alichukua hicho kizingiti kinachouunganisha Mbinguni, nami natumaini ya kwamba sisi sote tutakutanika huko siku fulani.

Na sasa nilinena hivi majuzi—nikasema, “Mwajua naamini ya kwamba nitakatiza jumbe zangu za Jumapili kufikia kama dakika ishirini na thelathini, kisha niwaombe wagonjwa.” Nami niliwaza hayo asubuhi ya leo, nami nikafikiri usiku wa jana wakati Dada Downing aliponipigia simu na kusema—akampigia simu Billy na kusema ya kwamba yeye na Dada Ungren wakiendesha barabarani waliteleza barabarani na motokaa ikaharibika. Na Billy alipokuwa angali dirishani, yapata... (Sijui ilikuwa saa ngapi, labda usiku wa jana wakati fulani; nilikuwa nimelala kwa muda mrefu kidogo). Nikaangalia kwa Ndugu Wood; taa zilikuwa zimezimwa. Nikapiga tu magoti kuomba, na nilipofanya hivyo kitu fulani kikaniambia, “Ni sawa.” Kwa hivyo basi nikamwambia Billy, “Mwambie kila kitu, nilifikiri, kingekuwa shwari.”

Nina furaha sana kuwaona humu asubuhi ya leo. Wakiketi katika nyumba ya Bwana humu nyuma baada... barabarani... Watu unaowapenda sana wanaosafiri maili mia kadhaa kusikia Injili; kisha nikawazia, ujumbe wa dakika ishirini nami ninavyonena pole pole, hautawafaa kitu. Kwa hivyo nikafikiria tu nita... urefu kama huo.

Kwa hivyo basi nilimsikia Ndugu Ungren, mwanawe, asubuhi ya leo alikuwa akiimba, “Jinsi Wewe Uliavyo Mkuu.” Yeye ana—inamaanisha mengi zaidi kwake asubuhi ya leo kuliko ilivyofanya jana aduhuri, kwa maana Mungu mkuu wa Mbinguni aliyahifadhi maisha ya mpendwa mamaye na dada yake wadhamani.

Sasa, leo tunatazamia wakati mkuu katika Bwana, nami nilikuwa na mafungu mawili ama matatu mbalimbali hapa niliyokuwa nikiyatazama, na singalijua nizungumzie lipi asubuhi hii. Moja lilikuwa *Mtwiken* *Yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Basi iwapo Yeye huwajali, nanyi je?* Kwa hivyo basi, lingine... wakati Billy Paul... ama si Billy Paul, mwanangu, Joseph, aliniletea fungu hili muda mrefu uliopita. Nilikuwa nimeketi chumbani siku moja, naye akasema—akiinua macho yake kuitazama picha, (naye Billy... Joseph anapenda mitumbwi sana kama vijana wadogo—mitumbwi na farasi, mwajua) naye akaniambia, “Baba, Yesu ana mtumbwi?”

Nami nikasema, “Sijui.”

Kwa hivyo basi, alipoamka na kuondoka nikawazia, “Je, Yeye ana mtumbwi?” Nami nikatoa somo hapo, nikaliandika hapa kwenye kitabu changu: *Je, Yesu Ana Mtumbwi?*

Nikafikiria wakati alipokuwa hapa duniani ilimbidi kuazima tumbo la uzazi apate kuzaliwa, kaburi la kuzikiwa, mtumbwi wa kuhubiria, bali Yeye ndiye Nahodha wa ile meli ya kale ya Zayuni. Anao bila shaka. Lakini katika vile vifungu nilivyokuwa nikifikiria—nikawazia labda ningevipata baadaye, kabla hatujaondoka kurudi.

Mwajua, napenda kuzungumza hapa Maskanini, kwa sababu ni kanisa letu wenyewe. Tunajisikia huru kusema cho chote Roho Mtakatifu asemacho. Katika mahali pengine, hata ingawa mtu huyo ataka ujisikie huru, unajisikia umesongwa kidogo kwa sababu uko katika kanisa la mtu mwingine, nawe unataka kuwa muungwana kutosha kuheshimu mawazo yao na mafundisho yao.

Nilikuwa na wakati wa ajabu juma hili huko chini mahali pa Ndugu Burcham. Nilienda katika kiwanda wanakatengeneza jibini. (Namwona yeye, mkewe, mwanawe, na wengineo wamo humu asubuhi ya leo.) Kila mara nimefikiri kiwanda cha jibini kingekuwa kama mahali pengine nimetembelea. Lo, panapoteleza na pachafu. Jamani, naweza kusema jambo moja, waweza kutosheka ya kwamba mahali hapo si pachafu. Hapo ndipo mahali pasafi sana nimewahi kutembelea, hasa katika kiwanda. Nami sikujua—Nilifikiri lo, labda wanatengeneza pauni mia moja za jibini kwa siku, nao wanatengeneza tani sita kila siku!—viwanda vitatu vikifanya kazi. Nikawazia, “Lo, jamani, nani anayekula jibini hizo zote.” Lakini Bwana amambariki mtu huyu nami nilipata majaliwa ya kuwa nyumbani kwake, nyumba ya kupendeza—mke mwema aliyejiweka wakfu. Na hamna subabu kwa kila siku kama wanavyofanya. Nilikutana na mwanawe, ni watoto wazuri sana. Tunashukuru sana kwa ushirika huu tulio nao sisi kwa sisi.

Nikaona kwamba mchungaji wao wa zamani ni mtu nimjuaye—Ndugu Gurley, mtu mzuri sana wa imani ya United Pentecostal niliyekutana naye miaka mingi iliyopita—Jonesbro, Arkansas. Sikujua ya kwamba wao . . . huyo alikuwa mchungaji wake, hata hivyo.

Sasa, kumbukeni ibada za jioni hii, kisha Bwana akipenda, Jumapili ijayo tena tunatumainia kunena. Ndiposa Jumapili ifuatayo basi inanipasa kwenda Chicago; basi nitakuwa nje kwa muda fulani. Inanipasa kuwarudisha jamaa yangu nyumbani Arizona kusudi wapate . . . watoto waweze kujiandikisha shuleni tena, basi tutaacha kumsumbua mchungaji—kuchukua ibada zake. Kwa hivyo tunamshukuru sana Ndugu Neville kwa ajili ya ukarimu wake. Mwajua, nimekuwa nikimwalika naye ana . . .

Nampenda Ndugu...mtu wa namna hiyo ambaye hana hila; hana uchoyo—ni Ukristo halisi tu. Napenda hilo.

Basi, tutasoma baadhi ya Maandiko kisha tutayafanua, na sijui ni wakati gani tutakapotoka kwa hizi jumbe ndefu, bali nafikiri...nilikuwa nikizungumza hivi majuzi kuhusu kuzungumza kwa muda mrefu, na mtu fulani akasema, “Vema sasa, kama ulinena tu kwa dakika chache, nawe uzungumze kwa mafumbo hata hivyo, hatungeweza kufahamu kamwe.” Kasema, “Endelea tu kuzungumza, na halafu punde si punde inafahamika.” Yeye akasema...Kwa hivyo basi labda Bwana anatutaka tuifanye hivyo.

Hebu tuinamishe tu vichwa vyetu tena. Bwana, Neno Lako liko wazi mimbarani na tukitambua ya kwamba pana siku litafungwa kwa mara yake ya mwisho, kisha hilo Neno litafanyika mwili. Ndiposa tunashukuru kwa ajili ya wakati huu asubuhi ya leo, na utufungulie kwa Roho Mtakatifu Wako, yaliyomo katika Neno hili tutakalosoma. Hebu na Roho Mtakatifu atufunze leo mambo ambayo tunapaswa kujua, nasi basi tusikize kwa makini kila Neno, tulipime kindani, kisha na wale wanaosikiza kwa kanda, hebu na wasikize kwa makini, nasi na tupate kushika yale Roho Mtakatifu anayojaribu kutufunulia sisi, kwa maana tunatambua ya kwamba kama ukitupa upako, huo upako si wa bure; ni kwa kusudi fulani—upate kutenda kazi kwa manufaa ya Bwana. Na mioyo yetu pamoja na ufahamu wetu ufunguliwe, Bwana.

Na tuwe na uhuru wa kunena, na uhuru wa kusikia, na njia ya kuifikia imani kuamini yale ambayo tumesikia yakitoka katika Neno la Mungu, yapate kutupa Uzima wa Milele katika ile siku kuu ijayo. Tubariki leo; tuhukumu tunapokosea. Hebu na tujue makosa tuliyo nayo, na utubariki katika njia iliyo ya haki, tupate kujua tuifuate njia gani na jinsi ya kutenda katika ulimwengu wa leo, tupate kuleta heshima katika maisha yetu hapa kwa Yesu Kristo, aliyekufa apate kutupa Uzima katika maisha makuu ya baadaye. Twaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, nataka kusoma tu kutoka mahali pawili Maandikoni asubuhi ya leo, na pamoja panapatikana tu katika Kitabu cha Kutoka; bila shaka, pote pawili panapatikana katika Kitabu cha Kutoka. Pamoja, sura ya 13, na kifungu cha 21 na 22, na panapofuata ni sura ya 14, kifungu cha 10, 11, na 12. Sasa, nitasoma Kutoka 13:12.

BWANA naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa Nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku;

Ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu.

Basi, katika Kutoka 14 na kifungu cha 10.

Hata Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakainua macho yao, na tazama, Wamisri wanakuja nyuma yao; wakaogopa sana; wana wa Israeli wakamlilia BWANA.

Musa akasema, kwa sababu hapo...samahani. Wakamwambia Musa, Je! kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri?

Neno hili silo tulilokuambia huko Misri, tukisema, Tuache tuwatumikie Wamisri? Maana ni afadhali kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani.

Nitasoma vifungu vingine kadha

Musa akawaambia watu Msiogope... (Sasa sikizeni kwa makini hapa)...Musa akawaambia watu, Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa BWANA atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele.

BWANA atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya.

BWANA akamwambia Musa, Mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendele mbele.

Nawe inua fimbo yako, ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Israeli watapita kati ya bahari katika nchi kavu.

Nami, tazama, nitaifanya mioyo ya Wamisri kuwa migumu, nao wataingia na kuwafuatia, nami nitajipatia utukufu kwa Farao, na kwa jeshi lake lote, kwa magari yake na kwa wapanda farasi wake.

Na Wamisri watajua ya kuwa mimi Ndimi BWANA, nitakapokwisha kujipatia utukufu kwa Farao, na magari yake, na farasi zake.

Kisha malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao, na ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele yao, ikasimama nyuma yao.

Ikafika kati ya jeshi la Misri na jeshi la Israeli, napo palikuwa na lile wingu na lile giza, lakini lilitoa nuru wakati wa usiku; na hawa hawakuwakaribia hawa usiku kucha.

Musa akanyosha mkono wake juu ya bahari; BWANA akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao mashariki, usiku kucha, akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika.

Wana wa Israeli wakaenda ndani katika nchi kavu; nayo maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kuume, na mkono wa kushoto.

Na wale Wamisri wakafuatia, wakaingia ndani kati ya bahari, farasi zote za Parao, na magari yake, na wapanda farasi wake.

Ikawa katika zamu ya alfajiri, BWANA

akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri.

Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa kuwa BWANA anawapigania, kinyume cha Wamisri.

Neno la Bwana ni kuu sana, nzuri sana, hamna njia ya kuacha kulisoma. Linakuwa tu hai tunapolisoma. Nafikiri katika somo hili asubuhi ya leo, ingawa linanaswa kwa kanda, nataka kusema haya mwanzoni: inaonekana . . . najikuta mwenyewe . . . Na sababu yangu . . . Jana nilipokuwa nikisoma—nami nikalipata hili somo, basi niliwaza, “Mimi, Bwana akipenda, nitanena kuhusu hilo kwa sababu linanisukuma chini.” Nami natumaini linatusukuma sote chini tupate kuona, na itufanye kuinua macho yetu, na kusoma kidogo kulinganisha siku hiyo na siku hii.

Nataka kuchukua maneno matatu kwa ajili ya somo, na hayo ni: *Mbona Unalialia? Nena!* Mungu alimwambia Musa, hapa katika kifungu cha 15, “Mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendele mbele.” Na, *Mbona Unalialia? Nena!*

Basi, tuna somo halisi, nami nitajaribu kuharakisha upesi iwezekanavyo jinsi Roho Mtakatifu aongozavyo. Nataka kuwazia juu ya . . . ya somo hili la Musa kumlilia Mungu katika wakati wa shida, naye Mungu akimkaripia Musa, wakati shida ilikuwa ikiendelea. Na inaonekana ni jambo la kawaida tu, kwa mtu kulia, basi ni karipio jinsi gani kwa Mungu kugeuka na kumkaripia kwa kusema hivyo—kwa kumlilia Yeye. Inaonekana kama kwamba ni jambo gumu sana.

Wakati mwingi tunapoyatazama Maandiko kwa njia yetu wenyewe ya kuyatazama inaonekana gumu sana, bali tukisoma kwa bidii punde tu, tutaona ya kwamba Mungu mwenye hekima yote anajua kile hasa anachofanya. Naye anajua jinsi ya kufanya mambo haya na jinsi ya kumshughulikia mwanadamu. Anajua yaliyo ndani ya mwanadamu. Anamjua. Hatujui. Tunajua tu kwa akili zetu. Yeye anajua kilicho katika mwanadamu.

Musa alizaliwa kijana mwanamume aliye na kipawa. Alizaliwa nabii, mkombozi. Alizaliwa na vifaa hivyo ndani yake alipozaliwa, kama vile kila mtu ajaye ulimwenguni huzaliwa na vifaa hivi. Kama ninavyoamini kabisa katika kujua kwa Mungu

tangu awali, kule kuchaguliwa tangu awali—si eti kwamba Mungu anapenda mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba—bali akiwa Mungu, ilimpasa kujua, naye ajua mwisho tangu mwanzo. Mwaona? Kama hajui, basi Yeye si ye asiye na kikomo; na kama Yeye si asiye na kikomo, Yeye si Mungu. Kwa hivyo hakupenda, bila shaka, mtu ye yote apotee, bali Yeye, akijua ni nani atakayepotea, na ni nani hangepotea.

Hiyo ndiyo sababu—kusudi halisi la kuja kwa Yesu duniani kulikuwa kuwaokoa wale Mungu kwa kujua Kwake tangu awali aliwaona na akataka waokolewe, kwa sababu ulimwengu wote ulikuwa umehukumiwa. Sioni jinsi tungalifundisha hayo kwa njia nyingine ye yote ila kujua kwa Mungu tangu awali, na Biblia inasema dhahiri kwamba Yeye ajua mwisho tangu mwanzo na anaweza kuinena. Kwa hivyo, watu wanapojaribu kujifanya kitu wasicho, wanafanya muigizo tu, na hakuna budi watatambulikana. Dhambi zako hukupata. Huwezi kuzifunika. Kuna kifuniko kimoja cha dhambi. Hiyo ni Damu ya Bwana Yesu Kristo, na haiwezi kutumiwa isipokuwa Mungu alikuwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Hilo ndilo kusudi la hiyo Damu kumwagwa—si kukanyagwa, kufanyiwa mzaha, na kutaniwa, na kunenewa mabaya na kadhalika, ilikuwa kwa kusudi halisi. Hiyo ni kweli. Si ikachezewe; si ikaigwe kwa kusema kwamba dhambi zimefunikwa wakati hazijafunikwa, na hamna mtu anayeweza kufunikiwa dhambi isipokuwa jina lake liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yesu alisema Mwenyewe, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba, na wote Baba alionipa (wakati uliopita) watakuja Kwangu. Hiyo ni kweli.” Kwa hivyo hauwezi ukafanya maneno hayo yaseme uongo. Yako hapa kwa ajili ya Kweli, na kwa kurekebisha.

Naye Musa alizaliwa akiwa na karama; ya imani; Musa alikuwa na imani nyingi. Tunaiona baadaye ikitoka kwake. Naye alizaliwa katika jamaa kuu, kwa maana tunajua jinsi baba yake na mama yake na . . . walitoka kwa jamaa ya Lawi ambayo ndiyo hadithi inayotangulia haya katika Kitabu cha Kutoka, ikisimulia vizuri sana maisha ya mtu huyu mashuhuri. Naye alikuwa mmoja wa watu wakuu sana wa Biblia, kwa maana alikuwa mfano halisi wa Bwana Yesu.

Yeye alizaliwa katika uzazi wa kipekee sana, kama Bwana Yesu; alizaliwa wakati wa mateso, kama Bwana Yesu; alizaliwa kuwa mkombozi, kama Bwana Yesu; alifichwa na wazazi wake kutoka kwa adui, kama Bwana Yesu; naye akafikia wakati wa huduma yake kama Bwana Yesu. Alikuwa kiongozi kama Bwana Yesu; alikuwa nabii, kama Bwana Yesu; na alikuwa mfanya sheria kama Bwana Yesu.

Nasi twaona ya kwamba alikufa juu ya mwamba, na hapana budi alifufuka tena, na kila kitu... maana miaka mia nane baadaye alikuwa amesimama juu ya Mlima wa Kugeuzwa, akimzungumzia Bwana Yesu. Mwaona? Malaika wakamchukua. Hamna anayejua alikozikwa; hata ibilisi hakujua hilo. Hakika, siamini ya kwamba yeye alizikwa kamwe. Naamini ya kwamba Mungu alimchukua, naye akafa juu ya mwamba aliokuwa ameufuata siku zote za maisha yake. Naye alikuwa mfano mkamilifu wa Kristo. Alikuwa mfalme juu ya watu; alikuwa mfanya sheria, alikuwa mtu wa kuwahifadhi watu; alikuwa kila kitu katika mfano wa alichokuwa Kristo.

Sasa basi tazama ya kwamba alizaliwa akiwa na karama yake kuu na sifa ndani yake. Bali ilichukua tu kitu fulani kukimulika kukifanya kitu hicho Hai. Mnaona, mbegu ya Mungu hakika iliwekwa ndani yetu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na wakati hiyo Nuru inapogusa hiyo mbegu, inaifanya Hai, bali Nuru haina budi kwanza kuiangazia ile mbegu.

Kama vile nimefundisha mara nyingi juu ya maskini mwanamke yule kisimani—yeye akiwa katika hali hiyo. Ingawa yeye alikuwa mtu mwenye sifa baya, ingawa maisha yake yalikuwa yameshushwa, naye alikuwa katika hali hiyo—kwa sababu mapokeo hayakuwa yamemguza kamwe. Ingawaje, wakati hiyo Nuru ilipomgusa kwanza, mara akaitambua, kwa sababu kulikuwemo kitu fulani mle kuiitikia.

Kilindi kinapopigia kelele kilindi, hapana budi kuwa na kilindi kingine mahali fulani kuitikia mwito huo. Naye Musa hapa alizaliwa huyu nabii, bali alilewa katika shule ya wenye akili na nyumbani mwa Farao. Farao Seti, aliyelewa chini yake, alikuwa mtu ambaye bado alikuwa mwenye kuheshimu na aliamini Yusufu kuwa nabii wa Mungu. Bali akaja Rameses baada ya Seti, na Rameses hakumjali Yusufu. Na kwa hivyo, hapo ndipo shida ilipoanza sasa—palipoinuka Farao asiyemjua Yusufu.

Bali sifa hizi kuu—hebu tuzungumze habari zake kwa muda mdogo tu kabla hatujaingilia sehemu muhimu ya somo hili. Nina njia ya kipekee ya kuanzisha somo na kulifafanua, na Bwana atusaidia asubuhi ya leo tunapolifafanua.

Musa alizaliwa na hii karama kuu ya imani, kisha akatiwa mafuta na kuagizwa kwenye Kijiti Kilichowaka Moto kuwakomboa watu wa Mungu. Naam, oneni jinsi mtu huyu alikuwa na sifa nyingi! Yeye alizaliwa kwa ajili ya jambo fulani. Mungu alikuwa na kusudi kwake. Mungu ana kusudi kwako kuwa hapa. Waona? Iwapo unaweza tu kuwa... kufikia mahali hapo, ni shida nyingi vipi utamwondolea Mungu pamoja nawe, pia.

Musa akazaliwa, (kisha alikuwa) baadaye akaletwa mahali alipotiliwa mafuta. Na tazama mbegu ile imekaa pale kwa mawazo ya kiakili, pamoja na imani yote aliyojaliwa nayo kuwakomboa watu hawa, hata hivyo haikuwa Hai hata hiyo Nuru kutoka kwa Kijiti Kilichowaka Moto ilipoimulika—hata alipoona, si kitu ambacho alikuwa ameshasoma habari zake, bali kitu alichokuwa ameona kwa macho yake—kitu kilichomzungumzia, naye akakizungumzia. Lo, jinsi hilo lilifanya mambo yawe Hai.

Nafikiri mtu ye yote mwenye... ama mwanamke, mvulana au msichana—na ninafikiri katika mawazo ya kiakili ya yale wanayodhani Neno lilivyo na kadhalika, hawawezi kamwe kuwa na msingi imara hata watakapokutana na hiyo Nuru ambayo hulifanya Neno kuwa kweli.

Nafikiri hamna kanisa katika taratibu zake, haidhuru ni la kibusara na asili vipi, kanisa hilo haliwezi kusitawi hata ya kimbinguni yamejulikana miongoni mwa watu wale, nao wayaone—kitu fulani wanachoweza kuzungumzia na kitawajibu na ambacho huthibitisha Neno hili lililoandikwa.

Sasa kumbuka, Musa alipokutana na hiki Kijiti Kilichowaka Moto hilo Neno lilithibitishwa kabisa. Ilikuwa Neno. Haikumpasa Musa kujisumbua, “Sauti hii inamaanisha nini? Hiki Kiumbe hapa ni nini?” Maana tayari Mungu aliisha andika kwenye Maandiko katika Mwanzo ya kwamba, “Watu wako watakuwa wageni katika nchi hii ya kigeni, bali watarudishwa baada ya miaka mia nne—watarudi nchini humu tena, kwa maana haujatimia uovu wa Waamori bado.”

Basi mamia na mamia ya miaka kabla Mungu hajasema ya kwamba Israeli watakuwa Wageni na kudhulumiwa katika nchi ya kigeni na wangekaa humo miaka mia nne, bali Mungu, kwa mkono wenye nguvu, angewatoa. Kwa hivyo unaona kwa hiki Kijiti Kilichowaka Moto, Musa alijua haya kiakili, na ile mbegu iliyojaliwa ndani yake ilikuwa moyoni mwake. Naye akajaribu kupitia ujuzi wake wa kiakili pamoja na kujaribu Neno kuwatoa—kuwakomboa, kwa maana alijua alizaliwa, kwa kusudi hilo. Alijua huo ulikuwa wakati ambao Maandiko yote yalisema wao tayari walikuwa wamekuwa huko kwa miaka mia nne.

Ni kama vile tunavyojua sasa, kama mtu fulani alivyoniuliza muda mchache uliopita kuhusu kule kuja na Kunyakuliwa. Tunajua ya kwamba wakati umekwisha. Wakati wa Kunyakuliwa umewadia. Nasi tunatazamia “imani ya kunyakuliwa” inayoweza kuunganisha kanisa na kulipa nguvu fulani za kimbunguni zinazoweza kuigeuza mili hii tunamoishi. Tunamwona Mungu anayeweza kumfufua aliyekufa akainuka kutoka sakafuni, ama nje uwanjani na kumfanya hai tena na kumleta mbele zetu. Tunapomwona Mungu anayeweza

kuchukua kansa ambayo imemla mtu akawa kivuli, na kumwinua akawa mtu mwenye nguvu na afya, hiyo inapaswa kuwapa watu “imani ya kunyakuliwa.” Ili kwamba wakati hiyo Nuru itakapomulika kutoka angani, na parapanda ilie, ule Mwili wa Kristo utakusanywa pamoja na kubadilishwa katika dakika moja na kuchukuliwa Mbinguni.

Naam, lazima kitu kama hicho kitendeke, na shule zetu za theologia haziwezi kamwe kutoa hayo, ingawa wao ni sawa kiakili, bali huna budi kukutana na hiyo Nuru! Huna budi kupata hicho kitu.

Na hapa Musa akiweka msingi wa wito wake juu ya Neno, (na ulikuwa mkuu) hata siku moja akakutana na Nuru hii, na Neno lenyewe likazungumza naye. Basi akapata upako wake. Huyu mpakwa mafuta, kilichokuwa ndani yake—kile kilichokuwa ndani, akili zilizoamini, imani ile iliyowekwa msingi juu ya imani ya Mungu ambaye alimtenganisha na mama yake. Na sasa alipofika kwenye hiyo Nuru, ikatia upako hiyo hata akaamini. Waona?

Ni upako jinsi gani, naye akaagizwa. Sasa, tunajua kwa kiakili alimsikiza mamaye. Alijua yale ambayo yangetendeka, naye alijua alikuwa akiishi katika siku hizo. Bali hapa akatambua kwamba yeye alikuwa ameshindwa, kwa hivyo huenda aka... imani yake huenda ilikuwa imefifia kidogo. Bali sasa alipofika kwenye kile Kijiti, Mungu akasema, “Nimesikia kilio cha watu Wangu, nami nakumbuka ahadi yangu kwa baba zao, Ibrahimu, Isaka na Yakobo, nami nimeshuka.”

Mimi, hicho ni kijina cha mtu binafsi “Mimi nimeshuka niwaokoe.” Na sasa, hebu niongeze tu hili kama lita... Mungu anisamehe iwapo inasikika kama kukufuru. “Mimi sitendi kazi duniani kupitia tu kwa mwanadamu. Mimi ndimi Mzabibu; nanyi ni matawi, na Mimi hujijulisha Mweyewe tu ninapoweza kumpata mtu, na Mimi nilikuchagua wewe, na nakutuma uende kule ukawatoe.” Mwaona? Sasa tazama, “Nitakuwa pamoja na mdomo wako nami... chukua hii fimbo.”

Naye Musa akasema, “Je, naweza kuona thibitisho ya kwamba utanituma nawe umenitia mafuta na utafanya mambo haya?”

Kasema, “Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?”

Akasema, “Ni fimbo.”

Kasema, “Itupe Chini”—nayo ikawa nyoka; yeye akakimbia.

Akasema, “Mchukue”—naye akageuka kuwa fimbo tena. Kasema, “Tia mkono wako kifuni mwako”—akautoa, nao ulikuwa na ukoma; akaurudisha, nao ukaponywa. Kasema aliona utukufu wa Mungu.

Hapakuwepo maswali mengine kwa Musa. Je uliisha kuona, yeye hakukimbia jangwani tena? Alijua alikuwa mpakwa

mafuta. Alijua mambo haya yote yalikuwa moyoni mwake. Hizi sifa nzuri, nazo zilikuwa na upako. Sasa yeye yuko tayari. Yuko tayari kwenda; kwa hivyo ndiye huyo akielekea Misri. Mungu alikuwa amesema, “Nitakuwa pamoja nawe,” kwa hivyo hilo lilitosha. Kama “Nitakuwa pamoja nawe,” ndiyo tu Musa alipaswa kujua kwa ajili ya mwito huu mkuu moyoni mwake. Na sasa, Mungu alisema, “Nitakuwa pamoja nawe.”

Naam, Mungu pia alikuwa amethibitisha dai la Musa. Musa alidai, “Nalikutana na Bwana.” Naye akasema, “Niwaambieni MIMI NIKO amenituma.” Mwaona?

Basi wakasema, “Hapa kuna mtu, Myahudi mwingine, labda baadhi ya hawa washupavu wa dini ambao wamekuwa wakija wakati wote wakiwa na mpango fulani wa kututoa utumwani.” Nanyi mwajua jinsi watu walivyo wanapokuwa watumwa ama utumwani kwa ajili ya jambo fulani, kila mara kuna mjaja fulani anaowajia, mwajua, kutenda hayo. Kwa hivyo Musa—Mungu alimwahidi Musa, “Nitakuwa pamoja na wewe; nitakuwa ndani yako. Maneno Yangu yatakuwa maneno yako. Basi nena maneno Yangu, na useme tu nisemayo.”

Na sasa Musa aliposhuka akaenda na kuwatolea mwito huu na kusimama mbele ya Farao na kumwambia Bwana Mungu wa Waebrania amesema, “Watoe hao wana,” naye hangewaacha waende. Kwa hivyo akafanya ishara mbele ya wazee na mbele ya Farao, na ishara alizoitenda Mungu.

Akasema, “Basi kesho wakati kama huu jua litatua. Kutakuwa giza katika Misri nzima.” Na ikawa hivyo, vivyo vivyo hasa. Ndiposa akasema, “Kutakuwa inzi juu ya nchi,” naye akainyosha fimbo yake na kuwaita inzi, nao nzi wakaja. Naye akatoa unabii, na kila kitu alichotolea unabii kikatendeka jinsi hasa . . . ilikuwa Mungu. Mwaona?

Mungu alikuwa amemwita tangu alipozaliwa, akaweka sifa ndani yake za imani kuu, kisha akashuka katika uwepo Wake na kutia mafuta kitu hicho kikuu ndani yake na akamtuma kule na Neno Lake, naye alikuwa amethibitishiwa kabisa madai yake. Haidhuru ni walaghai wangapi waliinuka, ni mangapi ya mambo haya mengine yalikuwa yametendeka; Mungu alikuwa akinena, na Musa alitambulishwa. Musa . . . Yale aliyosema Musa, Mungu aliyaheshimu! Nawatakeni msisahau kamwe hilo Neno. Yale aliyosema Musa, Mungu aliyaheshimu, kwa maana Neno la Mungu lilikuwa ndani ya Musa. “Nitakuwa pamoja na Mdomo wako. Utanena mambo ya kweli.”

Sasa, mambo asemayo Mungu, anayonena kupitia kwa Musa, na hiyo iliimarisha na kuthibitisha madai yake.

Pia, aliambiwa na mama yake kuhusu uzazi wake usioelezeka, na jinsi wakati ulikuwa umewadia karibu na ile saa ambapo kungekuwa na mkombozi. Amramu na Yokebedi, mwana na binti wa Lawi, wakaanza kumwomba Mungu

kumtuma mkombozi. Na inachukua...unapoona wakati wa ahadi umekaribia, inawafanya watu waanze kuomba na kuona njaa. Hapana shaka Yokebedi alikuwa amemwambia mara nyingi (mama yake—alikuwa mwalimu wake pia kama tujuavyo hiyo hadithi—naye alikuwa amemwambia jinsi alikuwa ameomba. “Na, Musa, ulipozaliwa, mwanangu, ulikuwa mtoto maalum. Ulikuwa tofauti. Kuna kitu kilichotendeka katika kuzaliwa kwako.”

Niliwafanyia watoto mchezo wa kuigiza si muda mrefu uliopita wakati Amram alipokuwa chumbani akiomba, alimwona Malaika akichomoa upanga wake na kueleleza kaskazini na kusema, “Utapata mwana, naye atawapeleka wake wana upande wa kaskazini hata kwenye Nchi ya Ahadi.” Nikiwaonyesha watoto wadogo mchezo wa kuigizwa kusudi wapate kuelewa. Akili zao hazijafikia mahali mlipo ninyi watu wazima, ambapo unaweza kufahamu mambo ambayo Roho Mtakatifu huwafunulia.

Sasa, ingawa mamaye alimwambia mambo haya na alijua haya, hata hivyo alihitaji kuguswa tena. Mafundisho yalikuwa mazuri, bali alihitaji mawasiliano ya kibinafsi.

Hayo ndiyo ulimwengu unayohitaji leo. Hayo ndiyo kanisa linayohitaji leo. Hayo ndiyo kila mtu anahitaji, kama wana na binti za Mungu. Ili uwe hivyo, unahitaji mawasiliano ya kibinafsi. Waona? Kitu fulani, haidhuru...unajua Neno ni kweli; unajua ni sahihi. Lakini basi linapowasiliana, ndiposa unaona jambo hilo limetendeka, ndipo unajua uko katika njia ya kweli. Waona? Na tazama, kila mara itakuwa ya Kimaandiko. Itadumu na Maandiko kwa sababu hii ilifanya hivyo.

Ombi la Amramu liliambatana kabisa na Maandiko. Maombi yao yanaambatana na Neno lililoahidiwa. Mungu aliahidi wakati huo kulifanya. Waliombea hilo, kisha hapa akazaliwa mtoto maalum. Na wao...

Tazama! Lo, jinsi ninavyopenda hili, waona! Katika ile saa Farao alikuwa akiwaua watoto wote, waona? Akiwaua kwa upanga, “upanga wa walezi”; waliwachoma upanga watoto hawa hata wakafa, wakawalisha mamba—hiyo miili midogo—hata mamba labda wakanona kwa miili ya watoto wa Kiebrania.

Bali Biblia ilisema ya kwamba hao wazazi hawakuogopa amri ya Farao kuwaua hao watoto. Hawakuogopa kwa sababu waliona kitu fulani katika mtoto huyu mchanga hapo awali. Walikiona, ya kwa hili lilikuwa jibu la maombi yao.

Na Musa alikuwa na haya malezi yote kwa hivyo Musa alijua alikuwa ametumwa kwa kusudi la kuwakomboa wana wa Israeli. Mnaona, malezi yote yanalundikana. Unapopata kitu cho chote na unaweza kuleta Biblia ukisema, “Hii itatendeka” na hapa inatendeka. “Hii itatendeka wakati huo,” na inatendeka.

“Hii itatendeka wakati fulani,” na hapo inatendeka, basi yote yanakusanyika pamoja na kutuchorea picha.”

Lo, jinsi haya Maskani asubuhi hii, jinsi sisi watu wa wakati huu, Ndugu Neville, tunapoona mvi zikiingilia nywele zetu na mabega yetu yakiinama, tunapoona ulimwengu ukijisokota-sokota na kuyumbayumba kama ulivyo, na jinsi tunavyoweza kutazama huku na kuona ile ahadi ikikaribia! Ni... Nafikiri wakati mwingi kama mtu ye yote angalirukia mara moja bila kulielewa—ama angalielewa hasa, aje kwake mara moja, nusura ingekupeleka katika Umilele, pamoja na tu... na jambo la kunyakulia kama hilo na halikujulikana kamwe. Ni, lo, pitia kwa mambo ambayo tumekwisha kuyaona, na kuyajua, na kuyafahamu, na yote yanatokea wakati mmoja. Mwanamume ama mwanamke, mvulana au msichana, labda watainua tu mikono yao juu na kusema, “Hebu twende, Bwana Yesu.” Mnaona? Lo, jinsi hiyo saa saa hiyo ilivyo karibu!

Musa akijua ya kwamba alizaliwa kwa kusudi hilo, alitazama madirishani na kuwaangalia hao Waebrania walipokuwa wakifanya kazi ngumu. Akayachunguza Maandiko hapa, yakasema, “Nao watakuwa wageni kwa miaka mia nne; (Waona?) bali nitawaleta kwa mkono wenye nguvu.” Halafu aliporudi baada ya agizo, ametiwa mafuta, yeye alijua ya kwamba alizaliwa—na imani yake, tazama—kwa imani akawaona hao watu na akajua walikuwa wana wa Mungu kwa maana Neno lilisema hivyo. Hawakuwa wa ulimwengu, hawakuwa kama wengine wao. Walikuwa tofauti. Nao walikuwa kombo na washupavu wa dini kwa uzuri wa kudanganya wa Misri, naye angekuwa mwana wa Farao, ambaye angetwaa huo ufalme baadaye, bali yeye...

Kulikuwa na kitu ndani yake, imani halisi ambayo haikuyatazama mambo hayo—zile anasa ambazo angerithi. Yeye alitazama ahadi ya Mungu, naye alijua ya kwamba wakati ulikuwa unakaribia. Na yale mtu huyo angaliwazia... Nataka kuzungumza naye habari hizo siku moja nitakapokutana naye kule ng’ambo.

Unasema, “Huo ni wazimu, ndugu...”

La, sivyo. Nitakutana naye kwa neema ya Mungu. Naam, bwana. Nitazungumza naye siku moja—Musa mwenyewe. Na jinsi ningetaka kumuuliza vile wakati alipoona kutayarishwa kwake, jinsi shetani angemhangaisha akisema, “Ahaa, hao watu hawatakuamini. Ahaa, hamna kitu kama hicho,” bali wakati hiyo mbegu ilipopata Uhai kule, kitu fulani kikamchapa, naye akajua kuna jambo fulani litatendeka. Alijua—akaangalia saa yake na kuona ilikuwa saa ngapi. Naye alijua. Jinsi alivyowaza alipokuwa akitazama.

Basi, alipoyaweka haya yote pamoja, mambo haya yote makuu aliyokuwa ameyaona—wakati wa Maandiko, maombi ya

mama yake na baba yake, naye alikuwa na uzazi wa kipekee, mtoto wa kipekee. Na daima kulikuwa na kitu fulani ndani yake, na sasa akaondoka na kujaribu kuwaza angejifunza uanajeshi katika shule yake na kuwakomboa wale wana, na hiyo haikufaulu. Kisha anaenda zake jangwani na kumwoa msichana mrembo wa Kushi, nao wakampata mvulana mdogo aliyelitwa Gershomu.

Na siku moja alipokuwa akichunga kondoo, mara akaona kijiti mlimani, kikiwaka moto. Naye akakwea kule na si mwenye akili, si kuwazia, si madanganyo, si madanganyo ya macho, bali ndani yake mlikuwemo Mungu wa Ibrahimu katika Nuru, Nguzo ya Moto kule nyuma katika kijiti—huo moto, kama mawimbi ya nuru yaliyokuwa yakitoka, bali haukukisumbua hicho kijiti. Na Sauti ya Maandiko, Sauti ya Mungu ikanena kupitia kwake na kusema, “Mimi, Mimi Nimekuchagua wewe, Wewe ndiwe huyo mtu. Nalikuinua kwa kusudi hili. Ninakuthibitishia hapa kwa ishara ya kwamba utawakomboa hao wana kwa maana Neno Langu halina budi kutimizwa.”

Lo, Neno Lake la wakati huu halina budi kutimizwa! Tunaishi katika wakati huo. Haidhuru mtu ye yote atasema nini, Neno halina budi kutimizwa. Mbingu na nchi zitapita bali si Neno Lake.

Basi, Musa alipoyaweka haya yote pamoja na kuona kila upande, iliitia upako imani yake. Amina! Lo jamani! Ni wazo jinsi gani. Hii, yenyewe, akaona kwa Maandiko ikionyesha kile ilichokuwa, na kule kunena kwa Mungu, na thibitisho lake pale, kuliitia upako imani aliyokuwa nayo, kwenda kutenda kazi. Inapaswa kutufanyia sisi nini!

Tunahitaji toba. Tunahitaji ufufuo. Ninasema *mimi mwenyewe*. Ninahitaji kutikiswa. Ninahitaji kitu fulani. Nilisema nilikuwa nikijizungumzia, ama kunena habari zangu mimi. Nahitaji kuzinduliwa. Na ninapowazia juu ya lile thibitisho kuu—kila kitu kiliwekwa pale vizuri sana. Na ikaitia upako imani ya Musa, kisha jamani, akaona hamna kitu.

Ndiye huyu akiitoroka Misri wakati bila shaka angalianzisha uasi ama cho chote kile, naye angaliasi na kuanzisha mapinduzi katika Misri naye angalichukua jeshi na kupigana, lakini mwaona... na alikuwa na maelfu kadhaa upande wake. Lakini badala ya hayo aliogopa hata kufanya hivyo—huku akiwa na jeshi upande wake. Lakini ndiye huyu akija miaka arobaini baadaye, mwenye umri wa miaka themanini huku akiwa tu na fimbo mkononi mwake. Mbona?—kilichokuwa kikiwaka moyoni mwake kiliishakuwa jambo halisi. Alitiwa mafuta wakati huo, naye alijua ya kwamba alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hamna kitu ambacho kingemzuia sasa. Hakuhitaji jeshi kamwe. Mungu alikuwa pamoja naye; hiyo tu ndiyo aliyohitaji—Mungu pamoja naye.

Lo, unapojua ya kwamba Mungu amekutuma kufanya jambo fulani, nawe unalionga likisongea pale, hamna kitu kinachoweza kupachukua mahali pake. Hivyo tu.

Nakumbuka nyakati ambazo Mungu ameniambia kuhusu mambo fulani ambayo yangetendeka, kisha nasonga mbele na kuyaona pale pale—lo, ni kujisikia kwa namna gani! Hivyo tu, mwaona? Kwa maana Mungu alisema hivyo.

Nakumbuka... Wengi wenu mnakumbuka kuhusu yule mvulana mdogo aliyefufuliwa kule Finland, halafu... kutoka kwa wafu, alikuwa ameuawa na motokaa. Nami nikasimama pale kando ya barabara na nikaanza kuondoka kwa mtoto huyo kisha nikageuka na kuangalia nyuma, na kitu fulani kikaweka mkono wake begani mwangu, nami nikafikiri ilikuwa Ndugu Moore—na hamna mtu aliyekuwa karibu nami.

Nami nikatazama nyuma, kisha nikainua macho yangu mlimani. Nikaona... Nikasema, “Vema, nimeona mlima ule mahali fulani, bali hatukupitia humu. Tulipitia njia nyingine. Ki wapi kile kilima?” Nami nikatazama nikaona hiyo motokaa kule chini imeharibika —nikamwona huyo mvulana mdogo pale mwenye... amelala pale “amenyolewa zaidi” (kama tunavyokuwa hapa); macho yake yamerudishwa nyuma kama ya Ndugu Way yalivyokuwa hivi majuzi alipoanguka; na maskini mguu wake mdogo umejipenyeza kwenye soksi ambapo viungo vyake vilivunjika; na macho yakitoka damu, na mapua, na maskio; kisha nikaona suruali yake fupi imefungwa kwa vifungo hapa kiunoni chake kidogo na soksi zake ndefu zimevutwa juu hivi kama tulivyokuwa tukizivalia miaka mingi iliyopita. Nami nikatazama pande zote, na ndiyo hiyo hasa—hasa jinsi Roho Mtakatifu alivyokuwa ameniambia miaka miwili hapo awali, wakati ninyi nyote mliandika katika Biblia zenu kote nchini ya kwamba hiyo itatendeka.

Lo, hapo... basi mambo yako tayari! Haidhuru yeye ni mfu jinsi gani; haidhuru mtu ye yote anasemaje; imekwisha. Hana budi kufufuka.

Nikasema, “Iwapo huyu mtoto hatafufuka kutoka kwa wafu, basi mimi ni nabii wa uongo; mimi simwakilishi Mungu vizuri; kwa maana katika nchi ya uenyeji wangu miaka miwili iliyokwisha, Yeye aliniambia haya yangetendeka.” Na hapo hawa wahudumu na kadhalika—imeandikwa katika ukurasa wa kwanza wa Biblia zetu, na ndiyo haya hasa. Someni toka kwa ukurasa wa kwanza jinsi itakavyotukia katika nchi iliyojaa miamba, na kadhalika—atauwa—atakuwa upande wa kulia wa barabara. Nikasema, “Ndiyo hii; hamna kinachoweza kuizua.” Mambo tayari yako shwari.

Imani iliyokuwa moyoni mwangu ilitiwa upako. Lo, jamani! Laiti tu ningaliweza kueleza hayo! Imani ambayo Mungu... niliyokuwa nayo katika Mungu ambayo iliniambia Yeye hawezi

kushindwa; ikaniambia, “Mambo yako shwari sasa. Hapa liko lile hasa nililowaonyesha miaka miwili iliyopita, na ndilo hili hapa katika utaratibu kabisa. Unachohitajiwa kufanya ni kunena Neno!” Naye maskini mvulana huyo akafufuka kutoka kwa wafu. Mwaona?

Nilikuwa nikifikiria na kutazama nyuma humu. Ndugu Fred Sothmann ameketi pale, Ndugu Banks Wood, na wengineo hivi majuzi kule Njia kuu ya Alaska, jinsi nilivyosimama kanisani na kuwaambieni ninyi nyote juu ya mnyama aliyonekana kama kulungu mwenye pembe zenye urefu wafuti arobaini na mbili na dubu mwenye rangi ya fedha na kijivu. Sijakuweko huko hapo awali na jinsi... ambavyo ningewapata hawa, na vile ingekuwa, na ni wangapi wangukuwa pamoja nami, na jinsi wangevalia. Mnajua hayo, kila mmoja wenu, majuma kadha kabla haijatatendeka.

Na pale, nilipoenda kule, bila kujua, yule mnyama alikuwa amelala pale. Nami nikaenda na yeye... haingaliwezekana, kama mwindaji angejua ama awe anasikiza kanda hii, jinsi ambavyo huwezi kwenda karibu na mnyama; angeruka na kukimbia. Bali hakufanya hivyo.

Ananing'inia pale katika chumba changu cha kusomea. Pale ananinginia yule dubu mwenye rangi ya fedha hasa vile tu... na rula imo mle, utepe wa kupimia kuonyesha hasa... na pembe itapungua angaa inchi mbili ama zaidi wakati ingali bichi juu ya mnyama na wakati inapokauka, bali hii haikupungua kamwe. Ingali hizo inchi arobaini na mbili kabisa. Mwaona? Pale yualala yule dubu mwenye rangi ya fedha, ana urefu wa futi saba hasa na kila kitu vile hasa ilivyokuwa, wako pale sasa.

Bali huyu mtu aliponiambia, “Sasa, tazama Ndugu Branham, tumempata huyu mnyama uliyenena habari zake lakini ulituambia ungempata dubu mwenye rangi ya fedha na kijivu kabla hatujafika chini ya kilima kurudi kule wale vijana wanaume—yule mwenye shati la kijani kibichi.” Nikasema, “Ni BWANA ASEMA HIVI. Mungu alisema hivyo.”

“Lakini Ndugu Branham,” yeye akasema, “naweza kuona kila kitu kwa maili kadhaa; hamna kitu. Atatoka wapi?”

Nikasema, “Hilo siwezi kuswali. Mungu alisema hivyo, Naye ni Yehova-Yire. Anaweza kumleta dubu pale. Angeweza kumweka mmoja pale.” Naye akafanya hivyo, na ndiye huyo.

Ni hali ya mambo inapokuwa shwari. Basi Musa alipoona ya kwamba aliinuliwa kwa kusudi hili naye alikuwa amekutana na huyo Mungu aliye mkuu uso kwa uso aliyekuwa ametoa ule mwito, naye akamtia mafuta, na kumtambulisha, na kusema, “Huu ndio mwito, wako, Musa. Ninakutuma. Nitakuonyesha utukufu Wangu, basi Ndimi huyu kwenye kijiti, kinachowaka moto. Nenda kule chini, nami nitakuwa pamoja nawe.” Hata

hakuhitaji fimbo. Alikuwa na Neno, Neno lililothibitishwa. Akaenda kule.

Ilitia upako imani aliyokuwa nayo. Nayo inatutia upako tunapoona ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, kuona ya kwamba hizi ishara zote tunazoonza zikitendeka. Zimeandikwa katika Maandiko ya kwamba zitatendeka katika siku za mwisho; kote toka Mbinguni hata kwenye nguvu za kisiasa, na tabia za watu, na upotovu wa ulimwengu na kati ya wanawake, na jinsi wangepanya katika siku za mwisho—na jinsi wanaume wangetenda, na jinsi makanisa yangetenda, na jinsi mataifa yangetenda, na jinsi Mungu angetenda. Nasi tunayaona yote yakiwa hapa nasi.

Lo, inatia upako imani yetu. Inatutoa katika duara kubwa, mwaona. Inatutenganisha na mambo yale mengine duniani, mwaona. Haidhuru sisi ni wadogo vipi; jinsi tulivyo wachache; jinsi tunavyochekelewa, kufanyiwa mzaha—haileti tofauti hata kidogo. Hivyo tu. Tunaiona. Kuna kitu fulani ndani yetu. Tulichaguliwa tangu awali kuiona saa hii, na hamna kitu kitakachotuzuia kuiona. Amina! Hapa, Mungu amekwisha kunena. Tayari imetendeka. Tunaiona. Jamani, jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa jambo hili! Lo! Basi inaleta imani yenu tunapoona mambo haya yakitendeka hapa.

Sasa, hapa tena tunasoma ya kwamba Musa alihesabu ya kuwa kushutumiwa Kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri. Naam, yeye alihesabu kushutumiwa Kwake Kristo. Sasa kumbukeni: *kushutumiwa Kwake Kristo*. Mwaona?

Kuna kushutumiwa katika kumtumikia Kristo. Kama unapendwa sana na ulimwengu, basi hauwezi kutumika—haumtumikii Kristo. La. Hauwezi, maana, waona, kuna shutuma inayoambatana nayo. Ulimwengu ulishutumu daima.

Kule nyuma kabisa maelfu ya miaka iliyopita, kulikuwa na shutuma iliyoambatana nayo. Naye Musa, ambaye angekuwa farao, (alikuwa halifa wa farao, mwana wa Farao), naye ndiye alikuwa Farao aliyefuata mwenye kibali mbele ya watu, na hata hivyo aliona kwamba (*kuhesabu* maana yake ni *kuona kwamba*)...aliona kwamba kushutumiwa Kwake Kristo ni mambo makuu kuliko yale yote Misri ingaliweza kumpa. Misri ilikuwa mikononi mwake. Bali alijua kuchukua njia ya Kristo ilikuwa shutuma, bali alifurahia sana kujua ya kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani yake, kilichomfanya aone huku kukaribia kwa Kristo...ama kushutumiwa kwa Kristo, hasa, ...kuwa ni kuuu kuliko anasa zote alizorithi. Alikuwa na urithi ndani yake uliokuwa mkuu sana kuliko yale urithi wa nje ulikuwa umempa.

Lo, laiti tungalikuwa hivyo leo na kumwacha Roho Mtakatifu atie mafuta hicho kilicho ndani yetu, hiyo imani, kufikia maisha ya kitaifa, yaliyowekwa wakfu kwa Kristo.

Basi, akiwa na imani kama hii aliyokuwa nayo, yeye aliona na kuhesabu huko kushutumiwa kama heshima.

Siku hizi mtu fulani asema, “Aisee, wewe ni mmoja wa wale watu? Wale ah...”

“Vema...aha...ha...;”

Unaionea aibu kidogo. Bali yeye alihesabu hiyo hazina kuu kuliko ulimwengu wote, kwa sababu kulikuwa kitu fulani ndani yake ambacho angalinena na kusema, “Naam, naheshimu hili. Hili limeheshimiwa sana. Nina furaha kuwa mmoja wao.” Mwaona? “Nafurahia kujihesabu mwenyewe kama Mwebrania na si Mmisri.”

Wakristo leo wanapaswa kusema jambo lile lile: “Nafurahi kujihesabu Mristo, kuepukana na mambo ya ulimwengu na taratibu za ulimwengu “—si mshiriki wa kanisa tu, bali Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anayeishi kulingana na Maandiko. Hata nikiitwa na washiriki wa kanisa “mshupavu wa dini,” hata hivyo nahesabu hiyo kuu zaidi... jambo kuu zaidi kuliko kama hata ningalikuwa mtu anayejulikana sana mjini ama taifani. Afadhali ningalikuwa hivyo kuliko kuwa Rais wa Marekani ama mfalme wa dunia, (mwaona?) Nahesabu hiyo kuwa juu zaidi, kwa maana Mungu katika rehema Zake kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu aliniona mimi na akaweka mbegu ndogo mle ndani kusudi imani yangu iruke juu ya mambo haya ya ulimwengu, na sasa ameniita, nami napahesabu mahali pangu—kama Paulo alivyosema alihesabu huduma yake—kuwa ni kuu sana. Lo, kwamba Mungu alikuwa amemwita asije akawa mwalimu mkuu kama Gamalieli, bali Paulo alikuwa ameitwa awe sadaka kwa ajili ya Kristo, waona.

Basi, jambo lile lile. Tazama, akiwa na imani kama hiyo hakutegemea kamwe kuona kwake—yale angalionga. Naam, hakuona kitu kule isipokuwa kundi la watu wanaoshikashika matope, watumwa, walio kifungoni, wakivawa kila siku, wakapigwa kwa mijeledi, wakadhihakiwa. Imani ya dini yao ilikuwa ushupavu wa dini. Na kulikuweko farao aliyeketi kwenye kiti cha enzi ambaye hakujua wala kujali kamwe dini yao. Hakujua chochote kuhusu...yeye ni kafiri, kwa hivyo yeye...

Ni picha ya namna gani ya leo. Na ndiyo hiyo, dini tofauti na jinsi kwamba kama huyu Musa, akiwa bado kwenye kile kiti pamoja na Rais ama yule mtu mkuu, Farao, kupachukua mahali pale baada ya kifo chake, naye alikuwa mzee. Hata hivyo Musa alifikiri ya kwamba huo mwito...alitazama kule nje. Na kwa dirisha lile lile Farao alilotazamia, kwa sababu alikuwa nyumbani kwake...Na Farao akatazama nje na kuona hao watu waliokuwa wameinua mikono yao, nao wangechukua mjeledi na kuwapiga hata wafe kwa maana walikuwa wakiomba. Wangaliwachoma kwa upanga kwa sababu hata walikosa

kutokutii wakati wo wote na kuwafanya wafanye kazi hata maskini miili yao ingedhoofika kabisa na kuwapa chakula haba. Vema, hawakuwa cho chote ila kundi la washupavu wa dini, hata ni vigumu kuwa wanadamu; hata hivyo Musa, hiyo imani ndani yake ikawaangalia, naye akasema, “Hao ni watu wa Mungu waliobarikiwa.” Amina. Napenda hilo.

Akiwa na imani kama hiyo... Macho yake hayakuona anasa za Misri; yaliona ahadi ya Mungu. Jicho lake la tai na la imani liliona ng'ambo ya hizo anasa za Misri. Anakumbuka anakuwa tai sasa; yeye ni nabii, na jicho lake la tai linainuka juu ya mambo hayo. Jamani, jinsi ninavyopenda hilo!

A-haa, jamani! Jinsi itupasavyo leo... Leo, Wakristo hutegemea hisi zao za yale wanayoweza kuona ama yale wanayoweza kufahamu, badala ya imani yao kutegemea yale unayoweza kuyaona kwa jicho lako na anasa. Kama ninyi wanawake—mimi daima huwasihi nikiwaambieni hamna budi kuachilia nywele zenu zikue; haiwapasi kujipaka rangi; hamna budi kutenda kama mabibi na Wakristo. Tazameni barabarani mkawaone wanawake siku hizi wamevalia kizinifu. Vema, unafikiria, “Vema, yeye ni mfuasi wa kanisa; mbona nami nisifanye hivyo?” Waona? “Na yeye anakata nywele zake; mbona siwezi kufanya hivyo? Vema, yuaonekana tu mzuri na mwenye akili... na utu ambao hata mimi mwenyewe sina. Lo, mbona nami nisifanye hivyo? Yanipasa kufanya hivyo.” Unapofanya hivyo, unaipooza imani yako. Waona? Hauipi imani yako nafasi ya kustawi. Anza na hilo.

Kama nilivyo sema... mtu fulani alisema, “Ndugu Branham, nchi—watu hukuchukua kama nabii. Haupaswi kuwa ukiwapigia wanawake kelele hivyo na pia wanaume juu ya mambo haya. Inakupasa kuwa ukiwafundisha jinsi ya kutoa unabii na kupokea karama.

Nikasema, “Nawezaje kuwafundisha hesabu ya herufi, na huku hawajui ABC zao?” Waona, sasa, anzia tu kwa hizo. Jitakaze mwenyewe, ili kwamba unapotembea barabarani unaonekana kama Mkristo kwa vyo vyote, waona? Na basi uendelee kutenda kama Mkristo, waona? Na hauwezi kufanya hivyo wewe mwenyewe. Inapaswa Kristo aje ndani yako, na iwapo hiyo mbegu imo mle ndani, na hiyo Nuru iiguse, itakuwa Hai. Kama haitakuwa Hai, hamna cho chote mle cha kufanywa Hai kwa maana bila shaka imejithibitisha kwa wengine, waona. Inakuwa hai mara hiyo Nuru inapoigusa.

Hilo ni karipio kwa wanawake, najua, wanaosikiza hii kanda ama watakaosikiza. Ni karipio kwako dada. Inapaswa kuwa hivyo! Inapaswa kuwa, kwa maana inaonyesha... Sijali umefanya nini. Huenda ukawa wa kidini maishani mwako mwote. Huenda uliishi kanisani. Huenda ikawa baba yako ni mhudumu, ama labda bwana wako ni mhudumu, bali mradi

tu unakataa kutii Neno la Mungu, inaonyesha hamna Uhai mle ndani. Unapoonza jambo hilo limefanywa dhahiri na Uhai wa Roho Mtakatifu, tazama itakapowaguzwa wengine. Ona yale wanayofanya. Kama inawaletea... si ajabu...

Ni karipio jinsi gani kwa wale Mafarisayo waliomwita Yesu—Yeye angetambua mawazo yao—wao wakamwita “Beelizebuli,” naye huyo maskini kahaba kasema, “Naam, mtu huyu ni Masihi. Maandiko yanasema Yeye atafanya haya.” Mwaona? Hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu awali ilikuwa mle, na wakati hiyo Nuru ilipoigusa, ikawa Hai.

Hauwezi kuuzuia, hauwezi kuuficha Uhai. Unaweza kuchukua...kumwagilia kokoto nyasini na kuiva wakati wa baridi. Katika majira yajayo ya kuchipuka kwa mimea wingi wa nyazi zako uko wapi?—ukingoni kuzunguka hiyo kokoto, kwa maana hiyo mbegu iliyo tayari kuchipuka chini ya hilo jiwe jua linapoonza kuangaza, hauwezi kuizuia. Itapenyeza njia yake kupitia kule na kujitokeza ukingoni mwake na kuchomoza kichwa chake kwa utukufu wa Mungu. Waona, hauwezi kuuficha uhai.

Jua linapoguzwa uhai wa mimea, haina budi kuishi. Na wakati Roho Mtakatifu anapogusa Uhai wa kimaandiko ulio ndani ya mtu unazaa matunda yake papo hapo. Kwa hivyo mbali na vile ulivyo wa kweli na mwaminifu, jinsi unavyosema wewe husemi...Kusema hawa wanawake wanaovalia hizi nguo mbaya na kadhalika kule nje, ambao ni wenda uchi wa kupindukia barabarani; ingawa hauamini ndivyo ulivyo, hauwezi kujifanya uamini. Unaweza kuthibitisha ya kwamba wewe hauna hatia ya uzinzi, bali katika kile Kitabu cha Mungu unafanya uzinzi. Yesu alisema, “Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Nawe ulijionyesha mwenyewe katika hali hiyo. Unaona, hauwezi kufahamu hayo isipokuwa Uhai huo umo mle.

Unamtazama mtu mwingine, na kusema, “Basi, namjua Dada Jones—Ndugu Jones ni muhuduma, mkewe hufanya hivi na hufanya vile.” Sijali hao hufanyaje, hili ndilo Neno.

Yesu alisema, “Neno la mtu ye yote liwe uongo, na Langu Kweli.” Ni Biblia, na wakati hiyo Nuru inapoigusa, haina budi kuwa Hai. Lazima iwe Hai.

Sasa, macho makuu ya Musa, jicho lake la tai lilitazama ng’ambo ya anasa za Misri. Mkristo aliye mwamini halisi leo, haidhuru kanisa husema nini, kile mtu ye yote asemacho, hiyo Nuru inapoigusa, wanaona thibitisho halisi la Mungu, hiyo Nguzo ya Moto ikining’inia pale katika ishara na maajabu yaliyoahidiwa katika Maandiko yakiwekwa kwake, inakuwa Hai. Haidhuru ni ndogo vipi ama lliyochache—kundi la Mungu daima limekuwa katika uchache. Waona?

“Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule Ufalme.” Waona? Wanaipata. Inampasa Mungu kuwatuma kutoka kila dhehebu, kila kundi, kila mahali, kuiona, iwapo wamekusudiwa Uzima.

Mtazame maskini Simeoni, aliyekusudiwa Uzima. Masihi alipokuja hekaluni, katika mfano wa mtoto mchanga mikononi mwa mamaye, Simeoni, kule nyuma chumbani mahali fulani akisoma, Roho Mtakatifu alimwinua, kwa sababu alikuwa akingoja. Uhai Huo ulikuwa ndani yake. Akasema, “Sitaona mauti hata nitakapomwona Kristo wa Bwana.” Na ndiye huyo Kristo wa Bwana hekaluni. Roho Mtakatifu alimtoa kazini mwake na kumwongoza kule naye akampokea huyo mtoto na kusema, “Mruhusu mtumishi Wako, aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yanauona wokovu Wako.”

Kulikuwa na mwanamke kizee, aliyekuwa kipofu pembeni, jina lake Ana, ambaye alimtumikia Bwana mchana na usiku. Naye pia alikuwa akibashiri na kusema “Masihi yuaja. Naweza kumwona akija.” Hata hivyo alikuwa kipofu, na wakati uo huo alipokuwa huko, huo Uhai mdogo uliokuwa ndani yake uliotabiriwa atakuweko; angekuweko; angekuweko. Basi Uhai uo huo, huo Uhai, ukaingia jengoni humo katika mfano wa mtoto mchanga kama mwana haramu, amevikwa nguo za kitoto, akipitia jengoni, naye Roho Mtakatifu akamgusa huyo mwanamke kizee aliyekuwa kipofu naye akaja kwa Roho, akaongozwa kwenye watu, hata akasimama mbele ya huyu mtoto mchanga, akambariki mama na kumbariki huyo mtoto mchanga, na akatabiri habari zake za usoni. Mnaona?—walikusudiwa Uzima. Mwaona? Watazame. Hapakuwa hata dazan yao.

Kulikuweko watu wanane tu waliookoka katika siku za Nuhu. Hao si wengi sana, bali wote waliokusudiwa Uzima walikuja wakati huo. Mnaona vile Roho Mtakatifu anavyofanya kazi katika kila wakati?—akiwavuta watu.

Sasa, tunaona ya kwamba imani ya Musa ilimwongoza kutazama yajayo, si yaliyokuwako. Tazama kesho, badala ya leo. Tazama ahadi, anasa. Watazame watu badala ya dhehebu. Waona? Mungu alifanya hayo.

Lutu angeona anasa za ufanisi kule Sodoma. Lutu angeona uwezekano wa fedha nyingi sana. Lutu angeona uwezekano alipotazama kule Sodoma na labda angekuwa...kwa kuwa alikuwa Mwebrania, huenda akawa mtu mkuu kule kwa maana alikuwa mtu mwenye akili sana na mpwake Ibrahimu. Kwa hivyo akachagua kuelekea Sodoma.

Akili za Lutu zilimwongoza kuona anasa za ufanisi. Akili za Lutu zilimwongoza kuona baraka za anasa. Bali imani yake ilipoozwa sana nazo, hata hakuona ule moto uliokuwa utaangamiza maisha kama hayo. Na hivyo ndivyo watu walivyo

sasa. Wanaona uwezekano wa kuwa wafuasi wa dhehebu kubwa. Wanaona uwezekano wa kuwa na cheo kati ya watu wa mjini, bali hawaoni ule uwezekano . . . Hawaoni—imani yao imepooza.

Hebu nirudie hiyo kusudi isieleweke vibaya. Wanawake leo, kama nisemavyo, wanataka kutenda kama wachezaji mashuhuri wa sinema. Wanaume leo wanataka kutenda kama wachezaji wa televisheni. Wahubiri siku hizi yaonekana wanataka kuyafanya makanisa yao kama vyumba mamboleo vya kupangisha vya aina fulani: wafuasi na kadhalika. Wanaona uwezekana wa kuwa labda askofu ama msimamizi mkuu ama kitu kama hicho kama wakiendelea na kanisa, wakisahau Maandiko huku yakiwa mbele yao pamoja . . . yamethibitishwa vilivyo na nguvu za Mungu na Neno Lililo Hai la Mungu, likiishi ndani ya watu. Hata hivyo hawalitaki. Wao husema, “Hatutaki kuchanganyikana na kitu kama hicho.” Ingeondoa kandi yao ya ushirika. Ingeondoa taratibu zao za kidhehebu. Hata hivyo mtu mwaminifu kama Lutu, akiketi chini kule Sodoma, akijua hayo ni makosa. Mnaona? Mnaona, wao wanafanya nini wanapofanya hivyo? Wanapooza ile imani ndogo *waliyokuwa nayo*. Haiwezi kutenda kazi.

Sasa, Musa aliacha hayo na akaelekeza imani yake—akaupooza ulimwengu. Au imani yako itazipooza anasa, au anasa zitaipooza imani yako. Naam, huna budi kuchukua moja au nyingine. Nawe waona Biblia haibadiliki; Mungu habadiliki. Yeye ni Mungu asiyebadilika.

Na sasa tunaona siku hizi ya kwamba watu wa siku hizi—waona, wao hutazama mambo yaliyo makubwa, madhehebu makubwa. “Mimi ni mfuasi wa *Fulani*,” waona? Nao wanaenda kule na tazama; hamna tofauti na watu wa barabarani. Hamna mambo mengine . . . Wana kitu cha kiakili fulani kidogo unachotaka . . . Unaponena kuhusu uponyaji wa Kiungu, Nguzo ya Moto, Nuru ya Mungu, wao wanasema, “Hayo ni mawazo.”

Mtu fulani alichukua ile picha ya Malaika wa Bwana hivi majuzi, muhuduma wa Kibatisti, na kuichekelea. Waona? Huko ni kukufuru. Waona? Hamna msamaha kwa hiyo.

Hivyo ndivyo alivyosema Yesu, waona. Ni kukufuru unapoiona ikitenda kazi zile zile alizotenda Kristo, naye alisema hao walipoona hizo kazi katika Kristo—Yeye alikuwa dhabihu—nao wakamwita “Beelizebuli,” shetani, kwa sababu alikuwa akifanya hivyo. Na sasa wao husema—Yeye alisema, “Nawasamehe hayo, bali Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, ukinena neno moja dhidi Yake, hautasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao.” Waona?

Neno moja tu ndilo unapaswalo kunena dhidi Yake. Waona? Ndiposa—kwa maana kama Uhai huo—iwapo umekusudiwa Uzima wa Milele, basi huo Uhai utabubujika utakapoiona. Utaitabua, kama maskini mwanamke yule kisimani na

wengineo; bali iwapo haimo mle, haiwezi kuwa Hai kwa kuwa hamna cha kuifanya Hai. Kama alivyozoea kusema maskini mama yangu, “Hauwezi kupata damu kutoka mboga nyekundu,” kwa maana hamna damu mle. Basi, ni jambo lile lile, nalo linaipooza imani haba uliyo nayo.

Lutu angeona zile anasa, bali hakuwa na imani ya kutosha kuona ule moto ambao ungeangamiza anasa kama hizo. Nashangaa kama tunayo leo? Nashangaa kama sisi...hao wanawake wanaotaka kupendwa na watu wote, wanaotaka kutenda kama wanawake wengine wa kanisa, kama wakiona ya kwamba wanataka kutenda kama wengine—wanaweza kuona uwezekano wa kuwa mwanamke mrembo zaidi kwa kujipaka rangi; wanaweza kuona mwanamke mrembo zaidi kwa kuwa na umbo la ujana kwa kukata nywele zao na kutenda kama wengine wa wachezaji mashuhuri wa sinema, bali nashangaa iwapo hiyo haijaipooza imani yao kujua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba mwanamke afanyaye hivyo ni mwanamke asiye na heshima. Na mwanamke anayevalia mavazi yanayompasa mwanamume ni chukizo mbele za Mungu—suruali ndefu na kadhalika na suruali fupi wanazozivalia. Imekuwa ukatili hivi kwamba hata limekuwa jambo la kawaida kwa watu wanaofanya hivyo. Nashangaa iwapo hao hawaipoozi ile imani haba kabisa waliyokuwa nayo hata kwenda kanisani. Mnaona? Hilo ndilo jambo ilifanyalo.

Lutu alifanya hivyo na ikampooza na kuwapooza watu wake kule chini. Hawangaliiona, bali Ibrahimu akiwa na imani iliyothibitishwa (mjomba wake), hakutazama zile anasa, hakutaka uhusiano wo wote nazo ingawa ilimlazimu kuishi maisha magumu na kujiishia mwenyewe pamoja na Sara—akaishi kule jangwani ambako alipata shida katika nchi yenye ukame, bali hao hawakutazama zile anasa wala uwezekano wa kupendwa na watu. Sara, mwanamke aliyekuwa mrembo sana nchini, Biblia ilisema hivyo. Ni mzuri, aliye mzuri sana katika wanawake. Na sasa yeye hata alikaa na kumtii mumewe hata alimwita bwana wake, ambaye Biblia humtaja hata katika Agano Jipya ikasema, “Nanyi ni binti zake mradi tu mnatii ile imani.” Mnaona—akamwita mumewe bwana wake.

Naye Malaika wa Bwana akazuru hekalu ama hema yao ndogo kule na akawaambia—hata hawakuwa na nyumba ya kuishi, waliishi huko nyikani, na ndivyo hivyo. Unaona siku hii imefananishwa tena kabisa na ilivyokuwa wakati huo?

Sasa, Musa kwa imani yake kuu tena angesema, “La” kwa mambo ya kisasa ya ulimwengu wa kisasa, na kufanya chaguo lenye haki. Hata alichagua kupata mateso pamoja na watu wa Mungu. Alichagua kwenda nayo. Kwa nini?—imani yake. Aliona ahadi; aliona wakati wa mwisho; aliona hata ya kesho, na akaachilia imani yake. Naye hakujali yale macho yake

yaliyoona katika uwezekano hapa kwamba yeye alikuwa Farao naye angekuwa farao, yeye alitazama hata akaona ya kesho.

Jamani, laiti watu wanalifanya hivyo! Hakuona ulimwengu wa sasa. Ukiutazama ulimwengu wa sasa, utauchagua. Yafiche macho yako toka kwake ukatazame ahadi ya Mungu, kule mbali katika mambo ya kesho. Kwa imani yake yeye angechagua. Alichagua kuitwa mwana wa Ibrahimu na akakataa kuitwa mwana wa Farao. Angewezaje hivyo, huku katika ufalme wote Misri ilikuwa imeshinda ulimwengu. Yeye alikuwa mfalme wa ulimwengu, akiwa kijana wa miaka arobaini hapa tayari kutawazwa, bali yeye hakutazama kamwe katika . . .

Tazama wanawake ambao wanalikuwa karibu naye siku kwa siku, wengi mno. Tazama hizo anasa, kuketi na kunywa divai na kutazama michezo ya kuvua nguo zao mbele yake huku wakicheza na kumpepea hewa—wanawake kutoka ulimwenguni kote, na vito na hazina na jeshi lake nje kule. Alichopaswa kufanya tu ni kuketi kitako na kula chakula chake kitamu na kusema, “Tuma jeshi kikosi nambari *fulani* humu kufanya *hivi na vile*; teka taifa hilo. Naamini nalitaka.” Hivyo tu ndivyo alivyopaswa kufanya: kuketi mle, nao wampepee hewa, na kuufungua mdomo wake, ndiposa wale warembo wenda uchi wa siku hizo wamwage divai kinywani mwake, wamlishe chakula chake huku wamemkumbatia kwa mikono yao—wanawake wote walio warembo sana ulimwenguni.

Anasa zote zilizokuwemo, zilikuwa papo hapo karibu naye, bali yeye alifanyaje? Alitazama mbali na hayo. Alijua moto ulikuwa tayari kwa hayo. Alijua mauti yalikuwa katika mstari huo. Waona? Alijua ilikuwa hivyo, na akatazama kwenye kundi la watu waliodhihakiwa na kukataliwa, na kwa imani yeye akachagua kupata shutuma za Kristo na akajiita mwenyewe, “Mimi ni mwana wa Ibrahimu; mimi si mwana wa huyu farao. Hata mkinifanya askofu, ama shemasi, ama askofu mkuu, ama papa, mimi si mwana wa kitu hiki. Mimi ni mwana wa Ibrahimu! nami najitenga na mambo ya ulimwengu. Amina, amina, na amina!

Kwa imani, alifanya hivyo. Akaondosha hizo anasa. Akaondosha uwezekano wa kuwa halifa wa askofu, akaondosha uwezekano wa kuwa halifa wa askofu mkuu ama mwangalizi mkuu katika uchaguzi ujao ama cho chote kile, akaondolea hayo mbali. Akakataa kuyaangalia.

Basi, “Nikiwa askofu, nitaingia. Watu watasema, ‘Baba Mtakatifu’ ama ‘Daktari *Fulani*’ ama ‘Mzee *Fulani*’. Jinsi wao . . . wahudumu wote katika kusanyiko hilo, watanipongeza na kusema, ‘Aisee, jamani, yule mtu ana kitu. Nawaambieni.’ Lo! ‘Sh-sh-sh, nyamazeni; hapa yuaja askofu.’ Waona? Asemayo, hayo ndiyo sheria. Waona? ‘Hapa yuaja *fulani*.’ Watu wataruka kwa ndege ulimwengu mzima kuwa . . . kumwona papa,

wambusu mguuni na pete na kadhalika. Ni uwezekano wa jinsi gani kwa Wakatoliki, ni uwezekano jinsi gani kwa Waprotestanti kuwa askofu ama msimamizi mkuu ama cho chote kile, mtu mkubwa katika dhehebu lao.

Kutazama...lo, lakini unaona jicho la imani huangalia mbele ya hayo. Nawe waona mwisho wake kule chini ambako Mungu anasema kitu hicho chote kitaangamizwa. Imani, hilo jicho la tai, linakuinua juu ya haya nawe unaona ya kesho, si ya leo, na kuchagua kuitwa mwana wa Ibrahimu.

Farao kwa kutokuwa na imani aliwaona watoto wa Mungu kama washupavu wa dini—bila imani. Aliwafanya watumwa kwa sababu hakuogopa aliyosema. Hakumwogopa Mungu. Alidhani alikuwa Mungu. Alidhani miungu yake aliyoitumikia—ambapo alikuwa askofu, alikuwa mwangalizi mkuu—mungu wake ndiye aliyefanya hivyo; hamna chochote kwa jambo hili hapa. Kwa hivyo akawafanya watumwa. Aliwachekelea—akawadhihaki kama tu watu wafanyavyo leo, jambo lile lile hasa.

Imani ya Musa iliwaona katika Nchi ya Ahadi, watu waliobarikiwa. Huenda ikawa ni vita vikali kuwaingiza kwenye nchi ya ahadi, bali Musa akachagua kwenda pamoja nao. (Jinsi ningalisisitiza hilo, bali wakati wangu unakwisha. Waona?)

Tazama, huenda ikawa jambo gumu kuwabadilisha watu hao. “Huna budi kwenda kuishi pamoja nao. Huna budi kuwa mmoja wao, nao tayari wana akili sana hata hauwezi kuwatikisa. Waona? Bali hapana budi jambo fulani litendeke kule. Hapana budi ya kimbinguni yaonyeshwe mbele zao. Litakuwa jambo gumu. Madhehebu yatakukataa, na mambo haya yote yatatendeka. Itakubidi kufanya mambo ya kutisha, hata hivyo, fanya chaguo lako.”

“Mimi ni mmoja wao.” Imani yake ilitenda hayo. Imani yake ikatoa spaki. Naam, bwana. Yeye aliiona.

Lilikuwa jambo gumu kuwapeleka kwenye hiyo ahadi, bali akafanya chaguo lake kwenda pamoja nao kwa vyo vyote. Bila kujali walimfanyia nini, jinsi walivyomkataa, alienda kwa vyo vyote naye alitoka pamoja nao.

Natumaini mnasoma! Sawa. Akaondoka akaenda pamoja nao kwa vyo vyote. Jifanye mmoja wao, hiyo ni kweli, kwa sababu ni wajibu wako. Labda mna vita vikali na mambo mengi utakayopitia, bali nenda kwa vyo vyote. Bali imani yake ilimwongoza kuchukua chaguo la Neno bali si anasa. Yeye alichukua Neno. Hivyo ndivyo imani ya Musa ilivyofanya.

Imani inapotazama walio wabaya sana wa Mungu—kumbuka, hapa ilikuwa ile anasa sasa—ulimwengu, aliye wa juu sana, mfalme wa ulimwengu. Na je, ahadi ya Mungu ilikuwa wapi?—kwenye shimo la matope, wakanyaga matope, bali wakati imani, wakati imani inapoangalia walio wabaya sana wa Mungu,

inawahesabu kuwa wa kuu sana na wenye dhamani kuliko yale bora sana ulimwengu uwezayo kuonyesha! Naam bwana,—imani inapowatazama, imani inapowaona.

Wakati imani katika Neno inapoweza kuona Neno limedhihirishwa, ni zaidi ya anasa zote na cheo cha askofu mkuu na kila kitu unachoweza kunena habari zake. Imani hufanya hivyo. Waona. Unaweza kuwaona walio wabaya sana, wanaodharauliwa, waliokataliwa, na cho chote kile; na wawe wabaya vipi, hata hivyo imani itawahesabu hao kuwa maili milioni moja juu sana kuliko yaliyo bora sana ulimwengu unapoweza kufanya. Amina!

Hivyo ndivyo tunavyoimba ule wimbo, “Nitaiendea njia ya watu wachache wa Bwana wanaodharauliwa...” Waona? Lo, jamani! Kwa kuwa, waona, imani huona yale Mungu anayotaka yafanywe.

Lo, natuamini haya yanaingia! Imani haiangalii wakati uliopo. Imani hailioni hili hapa. Imani hutazama kuona yale Mungu anayotaka, na kutenda kulingana na hayo. Hivyo ndivyo imani ifanyavyo. Inaona mahitaji ya Mungu, na yale Mungu anayotaka na imani hutenda kazi kupitia hayo.

Imani ni uonaji wa mbali. Haifupishi upeo wake. Hushikilia ionacho. Amina! Mpiga bunduki mzuri ye yote ajua hayo, Waona? Hiyo hulenga mbali; ni darubini kubwa, ni darubini ya macho ambayo haioni humu karibu; hutumii darubini ya macho kutazama ni saa ngapi. Waona? Huitumii hiyo, bali hutumia darubini ya macho kutazama mbali kabisa, nayo imani hufanya hivyo. Imani huitwaa darubini ya macho ya Mungu, zote mbili, pande zote mbili, Agano Jipya na Agano la Kale na kuona kila ahadi aliyofanya, nayo imani huona kule ng’ambo. Na imani huchagua hiyo, bila kujali wakati uliopo usemavyo hapa. Yeye hutazama kule mwisho.

Yeye hashushi darubini yake na kutazama upande huu; hutazama kule ng’ambo. Yeye huweka kipini cha kulengea shabaha katikati ya Neno kabisa. Hivyo ndivyo imani ifanyavyo. Hiyo ni imani iliyo ndani ya mtu inayofanya mambo hayo.

Sasa tazama. Tazama yale Farao aliyoitama... aliita... Yale Farao aliyoitama *makuu*, Mungu aliyaita *machukizo*. Farao huenda alisema, “Tazama Musa, hapa... naam, wewe ndiwe halifa wa Farao, nitakukabidhi hii fimbo ya mfalme niondokapo hapa. Nakukabidhi dimbo hii ya mfalme; ni yako.” Waona? Naam, hili ni jambo kuu. “Utakuwa mtu mkuu, Musa. Utakuwa askofu. Utakuwa *hivi*, na vile, ama... usituache. Kaa hapa.” Lakini mnaona, yeye aliita hayo mambo *makuu* naye Mungu akayaita *machukizo*.

Sasa, ninyi wanawake fikirini kwa muda mfupi—nanyi wanaume pia. Kile ulimwengu ukiitacho *kikuu* Mungu hukiita *uchafu*. Je, Biblia haisemi ni chukizo kwa mwanamke kuvalia

mavazi yampasayo mwanamume? Nawe unafikiri u nadhifu unapofanya hivyo. Waona? Unaonyesha mwili wa mwanamke kwa ajili ya shetani; hivyo tu. Kwa hivyo usifanye hivyo.

Ewe mwanamume unayeishia mambo ya ulimwengu na kushika na kukumbatia hili, nanyi wanaume msio na ujasiri wa kutosha kuwafanya wake zenu na kadhalika kuacha kufanya hayo: Hamna aibu. Mwajiita wana wa Mungu—kwangu yaonekana kama ulawiti kwangu. Mwaona. Si kuumiza dhamiri zenu, bali kuwaambia yaliyo Kweli. Upendo husahihisha. Kila mara hufanya hivyo.

Mama ambaye hawezi kumtuza mtoto wake, amkamsahihisha, na kumpiga, na kumfanya awe na tabia nzuri, yeye si mama kutosha. Hiyo ni kweli.

Sasa tazama yaliyotendeka basi. Musa aliona hili kwa ono lake naye Farao akasema kwamba, “Hili ni kuu.”

Mungu akasema, “Ni chukizo.” Kwa hivyo Mungu... Musa alichagua yale Mungu aliyosema.

Sasa tazama, imani huona yale Mungu anayotaka muone. Mwaona? Imani huona anachoona Mungu, na majadiliano na hisi huona yale ulimwengu unayotaka uone. Tazama, majadiliano... “Vema, hiyo tu ni hisi ya mwanadamu; sababu yake tu ni hii... Vema, si hii ni nzuri pia.” Waona? Ndivyo ilivyo hasa unapotumia hizo hisi ambazo ni kinyume cha Neno. Waona? Basi hayo ndiyo ulimwengu unayokutaka uone. Bali imani haitazami hayo; imani hutazama aliyosema Mungu, waona? Mwajua, tupilieni mbali majadiliano... Majadiliano... a—a... Hisi ya kujadiliana huona yale ulimwengu unayotaka uyaone—madhehebu makubwa.

“Je, wewe ni Mkristo?”

“Lo, mimi ni Mpresbeteria,” “...Mmethodisti”; “...Mlutheri”; “...Mpetekoste”; kadhalika. “Mimi ni *hiki, kile* ama *kinginecho*”—*hizo ni hisi*. “Mimi ni mfuasi wa Kanisa la Kwanza”; “Lo, mimi ni Mkatoliki”; “Mimi ni *hiki, kile*, au *kingineche*.” Waona?

Unasema hayo. Naam, hizo ni hisi. Unapenda kusema hivyo kwa sababu ni dhehebu, kitu kikubwa... “Tuna wafuasi wengi kuliko kanisa lo lote ulimwenguni, waona?” Bali kuna Kanisa moja tu halisi, hujiungi nalo; unazaliwa ndani yake. Waona? Na iwapo umezaliwa ukiwa ndani yake, Mungu Aliye Hai hutenda kazi kwako, akijifanya Mwenyewe ajulikane. Waona? Humo ndimo Mungu anamoishi—Kanisani Mwake.

Mungu huenda Kanisani kila siku—huishi Kanisani, Yeye huishi ndani yako. Wewe ni Kanisa Lake. Wewe ni Kanisa Lake. Wewe ni hekalu anamoishi Mungu. Wewe binafsi ni Kanisa la Mungu Aliye Hai. Na iwapo Mungu Aliye Hai huishi katika kiumbe Chake kilicho Hai, basi matendo yako ni ya Mungu.

Kama sivyo, basi Mungu hayumo mle. Hawezi kukufanya utende hivyo wakati anaposema katika Neno hapa, ramani Yake, “Usifanye hivyo,” nawe unafanya. Unaona, hilo ni kosa. Unapokana hilo, hiyo inaonyesha huo Uhai hata haumo ndani yako. Waona? Hiyo ni kweli.

Imani ilimwongoza Musa katika njia ya utii. Tazama, Musa alifanya... Hapo kuna Farao kijana; hapo kuna kijana Musa—wote wawili wakiwa na nafasi.

Musa aliona kule kushutumiwa kwa hao watu na akakuhesabu kuwa hazina kuu kuliko yale yote Misri iliyokuwa nayo; naye akiongozwa na imani. Alifuata yale imani yake iliyosema katika Neno nayo ikamwongoza kwenye njia ya utiifu na hatimaye Utukufuni. Asiyekufa—hatakufa kamwe—kwenye uwepo wa Mungu.

Kuona na hisi zilimwelekeza... na anasa zilimwongoza Farao kwenye kifo chake na maangamizi ya Misri, taifa lake na halijainuka tena tangu wakati huo.

Naam basi. Ukitazama *hili*, utakufa. Ukitazama *kile*, utaishi. Sasa, fanya chaguo lako.

Hilo ndilo jambo lile lile Mungu aliweka mbele ya Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni. Waona? Kwa imani huna budi kufanya chaguo lako. Sasa tazama, kuona kulimwongoza Farao mautini, na kwenye maangamizi ya jiji lake. Musa, kwa imani yake, hakumwogopa Farao kamwe. Waona? Hakujali aliyosema Farao. Hakumjali Farao zaidi ya mamaye na babaye walivyojali vitisho. Musa alipothibitishiwa kuwa ndiye, naye alikuwa mtu atakayeikomboa Misri—kuwaongoza Israeli kutoka Misri, hakujali aliyosema Farao. Hakumwogopa. Amina, amina, amina! Mnaona ninayomaanisha.

Hamna uoga katika imani. Imani inajua hayo. Imani kama nilivyosema daima, ina misuri mikubwa mno na malaika kifuni. Imani husema, “Nyamaza!” na kila mtu ananyamaza. Hivyo tu. “Najua nilipo!”

Wengine wao husema, “Vema, labda yeye yuajua.” Lakini inakupasa kusimama na kuonyesha misuri yako. Hivyo tu; imani hufanya hayo.

Tazama, Musa hakumwogopa Farao baada ya Mungu kuthibitisha mwito wake. Musa alipoamini ya kwamba ameitwa kufanya hivyo, bali Mungu alipomwambia kule, “Ndivyo ilivyo,” naye akashuka na kuonyesha mbele ya Farao na wengine wote ya kwamba alitumwa kufanya hivyo, Musa hakumwogopa Farao kamwe.

Angalia, Farao alitumia hekima yake juu ya Musa hata hivyo. Tazama. Alisema, “Hebu nikwambie, nitafanya mapatano pamoja nawe,” (baada ya kuliwa na yale mapigo) kasema, “Nitafanya mapatano nawe. Nendeni tu kwa ushirika mdogo

wa siku tatu. Mwenda umbali fulani, na msiende mbali zaidi.” Bali mwajua hayo yalikuwa yale hisi za Farao ziliyomwambia, Mwaona? “Nendeni umbali fulani lakini msiende mbali zaidi.”

Je, hatuna watu wa namna hiyo siku hizi? “Kama ukijiunga na kanisa, hiyo ni sawa.” Lakini, mnajua imani aliyokuwa nayo Musa haikuamini katika “dini ya umbali fulani.”

Yeye alisema, “Sote tutaenda. Tutaenda kabisa. Hiyo ni kweli. Tunaenda kwenye Nchi ya Ahadi. Hatuondoki kwenda hapa nje tukajiundie dhehebu na kukoma hapo, tutaendelea mbele kabisa.” Amina. “Naenda zangu kwenye Nchi ya Ahadi. Mungu alituahidia.”

Tuna Farao wangapi siku hizi wanaosimama mimbarani?—viongozi wa madhehebu. “Basi, ukifanya *hivi* na *vile*, hiyo yatosha. . . Vema, waona, umbali fulani tu.”

Bali Musa akasema, “Lo, hash! La, la, la, la.” Waona?

Farao akasema, “Vema, mbona—kama mtakuwa na dini ya aina hiyo, nitakwambia la kufanya. Wewe tu na wazee nendeni mkaabudu, waona? Wewe tu na wazee nendeni, mkaabudi, kwa sababu nyote mnaweza kuwa na dini ya namna hiyo, bali msiieneze miongoni mwa watu.”

Mnajua Musa alivyosema? “Hamna hata ukwato utakaoachwa nyuma. Tutaenda kabisa. Tutaenda sisi sote! Siendi kama wao hawaendi, na mradi tu niko hapa, nimo mikononi mwako! Amina. Siendi isipokuwa nao wanaweza kwenda pia. Hiyo tu.” Amina.

Jamani, ni mtumishi hodari vipi! Amina. “Nataka kuwachukua twende pamoja. Ati kwa sababu tu nimeipata—nami naketi kitako na kusema, ‘Hii ni sawa’—la, bwana; tunataka hao watu pia. Kila mmoja wetu ataenda.” Amina. Yeye akasema, “Nasi hatutaacha hata mmoja wa kondoo wetu wala chochote nyuma. Hakuna kwato itakayoachwa nyuma. Tunaenda kwenye Nchi ya Ahadi, (Amina)—kila mmoja wetu. Hata kama wewe ni mke wa nyumbani, ama u yaya mdogo, ama hata kama wewe ni mama kizee, ama kijana mwanamume, ama cho chote kile, tutaenda kwa vyo vyote. Hamna hata mmoja wetu atakayeachwa nyuma. Amina. Kila mmoja wetu ataenda. Hatutazuiwa na kingine chochote.” Hiyo ni kweli.

Jamani, hizo dini zilikuwa na mahojiano moto moto kule, sivyo? Lo, Jamani. Hasha, Musa hakuamini katika hii “dini ya umbali fulani tu.” La, hakuamini hayo. Naam, bwana. Lo, jamani. Tungedumu siku nzima juu ya hilo bali sina budi kurudia somo langu baada ya muda mchache na kuanza kuhubiri. Tazama.

Tazameni hili. Ni la kupendeza jinsi gani lo, napenda hili. Unajua hatimaye Farao alisema, “Tokeni!” Mungu alimpiga mapigo kwa sauti ya Musa. Alipiga kila kitu. Akafanya kila kitu

kilichopaswa kufanywa. Akakomesha... Akalifanya jua litue mchana katikati; akatenda kila kitu. Akautia mchana giza, akawaleta vyura, viroboto, chawa, kila kitu; moto, moshi na mauti kwa jamii yake na kadhalika. Akafanya kila kitu hata hatimaye Farao akalazimika kusema, "Tokeni! Chukueni mali yenu yote muondoke." Lo, jamani. Sifa ziwe kwa Mungu!

Nashukuru ya kwamba mtu anaweza kumtumikia Mungu hata shetani asijue la kufanya naye. Hiyo ni kweli. Akamtii Mungu kabisa hata shetani akasema, "Lo, jamani. Ondokeni. Sitaki kusikia hayo tena." Hiyo ni kweli. Unaweza kufanya hivyo—kabisa.

Unaona sasa, kama Mungu hangalimuunga mkono Musa, basi angalikuwa mtu wa kuchekwa, bali Mungu alikuwa hapo hapo akiithibitisha. Kila kitu alichosema kilitimia.

Naye Farao alipaswa kushikilia cheo chake kwa sababu alikuwa askofu mwajua, kwa hivyo ilimbidi kukaa kule. Hangeweza—hangalisema, "La," kwa sababu tayari ilikuwa ikitendeka. Waona. Hangeweza—hangeweza kuikana kwa sababu ilikuwa tayari inatendeka. Kwa hivyo hatimaye akasema, "Lo, ondokeni mwende; sitaki kuwasikieni tena. Ondokeni hapa; chukueni yote mliyo nayo muondoke." Lo, jamani.

Sasa, tunaona Musa, hapa, baada ya Mungu kumfanyia mambo mengi na kumwonyesha ishara nyingi na maajabu. . .

Naam, kwa dakika kumi na tano zifuatazo hebuni tufafanue hili hapa. Tazameni kwa makini sana.

Musa akafikia mahali hapa ambapo... Mungu alikuwa amesema, "Niko pamoja nawe. (Maneno yako ni Neno Langu, nimekuthibitisha, Musa. Ulikuwa kule wakati hapakuwepo inzi, inchini, haukuwa wakati wake.) Nawe ukasema, "Inzi waje," nao wakaja. Huo ni uumbaji. Ni nani awezaye kuleta giza duniani ila Mungu? "Ulisema, 'Iwe giza,' ikawa giza. Ulisema, 'Vyura na waje,' na vyura wakaingia hata katika nyumba ya Farao, vitandani, nao walipolundikana, mafungu makubwa... " Muumbaji... "Nami nimenena kupitia kwako, Musa, na kulifanya Neno langu liumbe kupitia midomo yako. Nimekufanya wewe mungu hasa mbele ya Farao." Naam, bwana. "Nimefanya haya yote, kisha wakafikia mahali"— majaribu madogo yakawapata, naye Musa akaanza kulia "Nifanyeje?"

Nawatakeni muone. Hili ni funzo kubwa sana hapa. Napenda hili, mwaona. Mnaona, Musa—kama tukisoma hapa vyema, mara hao wana walipoanza kuogopa—walimwona Farao amewafuata mbio wakiwa kwenye wajibu wao. . .

Mungu alikuwa amefanya kila kitu kikamilifu; sasa aliwatia safarini. Akalikusanya kanisa pamoja. Walikuwa tayari wameitwa watoke; walitoka katika kila dhehebu; wote wakaja pamoja. Musa akarudi kule nyuma na kusema, "Bwana, nikufanye nini?"

Yeye angesema, “Vema, nenda kafanye hivi. Vema, endelea. Sasa, Musa, unajua nimekuita kufanya hivi.”

“Naam, Bwana.”

“Vema, nenda ukasema haya; itakuwa”—ndio hawa inzi wakaja. “Nena kwa ajili ya hiki”—ndicho hiki hapa. “Fanya hivi”—hapa kinakuja. Kila Kitu kilikuwa BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI!

Basi, shida ikampata, naye Mungu anasema, “Basi, wameanza safari yao; wote tayari wameitwa watoke. Kanisa liko pamoja, kwa hivyo nimewaweka safarini. Basi Musa, waongoze huko. Nalikwambia la kufanya. Nitaondoka niende kule—niketi kitako nipumzike kwa muda mdogo.

Musa akasema, “Lo, Mungu, waone wakija humu! Ndiye huyu Farao anakuja! Watu wote... nifanyeje! Nifanyeje!” Angalia pale, si huo ni uanadamu tu. Naam bwana. Akaanza kulia, “Nifanyeje!”

Hapa tunamwona Musa akionyesha tabia ya mwanadamu kabisa—kila mara unataka Mungu aje nyuma yako na kukusukumiza kwenye jambo fulani. Naam, hiyo ni sisi siku hizi. Unataka Mungu baada ya kuona yote tuliyoona, unataka Mungu kukusukuma kufanya jambo fulani, waona? Musa alikuwa tayari amekuwa mzembe—kasema, “Mungu, nitakuuliza, nione utasemaje.”

“Naam, naam,” unasema, “Vema, sawa. Nitasema hivyo pia.” Waona?

Bali hapa Mungu alikuwa tayari amemtawaza kwa kazi hiyo, akathibitisha alikuwa pamoja naye, na ndiye huyu, mambo mengine yakazuka, kisha akaanza kulia, “Nifanyeje? Bwana, nifanyeje?”

Basi kumbuka, yeye tayari alikwisha kutoa unabii hapa, kwa maana alisema, “Hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena.” Kisha papo hapo akaanza kulia, “Mungu, tufanyeje?” Baada ya kufanya kazi nzuri sana katika kutabiri pale. Waona, aliisha waambia yale yangetendeka. Kama Neno la Mungu lilikuwa ndani yake, lilikuwa ndani yake. Na alipokuwa akisema hayo, bila shaka ikatendeka—aliyosema tayari yalikuwa yatatendeka, na ndiye huyu hapa akilia, “Nifanyeje?”

Lo, kama huo si uanadamu. Kama hiyo si mimi! Kama hiyo si mimi! Aliisha thibitisha, “Utakayosema yatatendeka. Mimi niko pamoja nawe.” Kisha hali ya mambo ilizuka kwa ghafula. “Nifanyeje? Nifanyeje Bwana? Ee Bwana, uko wapi? Ee, je, unanisikia? Nifanyaje?” Na tayari aliisha mchagua, akamthibitisha, na kumshuhudia na kufanya kila kitu kupitia kwake, na hapa—“Nina!” Jamani, anaionyesha kikamilifu.

Mwanadamu hupenda kustarehe na kumwacha Mungu amsukume. Na hata hivyo yeye alijua ya kwamba Mungu

aliisha kumpaka mafuta kwa ajili ya hiyo kazi, kufanya hivi, na Mungu aliisha thibitisha madai yake dhahiri. Ulikuwa wakati wa kukombolewa kwa hao watu. Mungu kwa miujiza yake na maajabu aliisha wakusanya wote katika kundi moja. (Mnanifuata?) Akawakusanya wote katika kundi moja—akathibitisha madai yake. Maandiko yalisema hivyo. Hapa kulikuwa ishara, hapa kulikuwa thibitisho. Hapa kila alichosema...kisha akaja miongoni mwao kama nabii. Cho chote alichosema, Mungu alikitimiza, hata kuumba na kuwaleta inzi na kufanya vitu viweko. Na kila kitu alichokuwa amemwahidia, hapa akakifanya. Bali alitaka kungojea BWANA ASEMA HIVI. Mwaona?

Ilimpasa kujua ya kwamba thibitisho dhahiri la wito wake lilikuwa! BWANA ASEMA HIVI. Kazi aliyochaguliwa ilikuwa BWANA ASEMA HIVI. Mnaweza kufahamu hayo? Mm! Mbona yeye alingojea BWANA ASEMA HIVI?

Yeye alitaka, “Bwana, nifanyeje? Hapa nimewaleta hawa wana umbali huu. Hali ndiyo hii: Farao yuafa; wote watakufa. Nifanyeje? Nilifanyeje?”

A-haa, a-haa, alikuwa tayari amebashiri kile watakachofanya. Aliisha kusema kile hasa watakachofanya. Alibashiri mwisho wa taifa alimolelewa. Natumaini mnafahamu. Tayari Musa alisha sema, “Hamtawaona tena kamwe. Mungu atawaangamiza. Wamewadhihaki muda mrefu kutosha. Mungu atawaangamiza.” Tayari aliisha bashiri yatakayowapata kisha “Bwana, nifanyeje?” Mnaona tabia ya binadamu hapo? Mwaona? “Nifanyeje? Nitangoja BWANA ASEMA HIVI.” Naam, bwana. “Nitaona yale atakayosema Bwana, kisha nitafanya hivyo.” Kumbukeni, kulikuweko na Farao...aliyekuwa ameinuka asiyemjua Yusufu, mwajua—wakati huo, wakati uo huo. Mwaona? Naye Musa akasimama na kutabiri mwisho wa taifa hilo. Naye ndiye huyu hapa mahali hayo yalipokuwa yakitendeka, halafu analia, “Nitafanyaje, Bwana? Nitafanyaje?” Mnaona?

Si hilo ni unadamu? Si hiyo ni tabia ya binadamu? “Nifanyeje?” Alikuwa tayari...ametabiri. Mungu alikuwa ameshatimiza kila kitu alichokuwa amesema, naye alikuwa ameitiwa kazi hiyo, kwa hivyo mbona ilimbidi kusema, “Nifanyeje?” Kulikuweko na haja, ulikuwa wajibu wake juu yake. Mungu alimtaka Musa kufanyiza kazi hiyo karama ya imani aliyokuwa amempa. Mungu alikuwa tayari amethibitisha. Ilikuwa Kweli, naye Mungu alitaka Musa—alitaka watu waone ya kwamba alikuwa pamoja na Musa. Naye, anangoja kule nyuma, kasema “Sasa, Bwana, mimi ni mtoto tu. Hebu uniambie sasa. Naam, nitaenda nikafanye hivi. Nina BWANA ASEMA HIVI.”

“Ndugu, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI?”

“Naam, naam, Ndugu Musa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.”

“Naam, sawa. Tumeipata sasa, BWANA ASEMA HIVI”—nayo ikatendeka. Haikukosa kutimia hata wakati mmoja. Haikukosea kamwe.

Ndiyo hii tena chini ya hali ya mambo, yakazuka tena. Naam, amewafanya washike safari. Kanisa tayari limeitwa litoke. Amewaingiza safirini, nao wana safiri. Naye Musa akaanza kulia, “Bwana, je, hii ni BWANA ASEMA HIVI? Nifanyeje mimi?”

Vema, Mungu alimtaka Musa kuwa na imani apate kuitumia hiyo karama ambayo tayari ameithibitisha dhahiri. Mungu alimthibitishia Musa pamoja na hao watu wazi wazi ya kwamba ilikuwa Yeye kwa Neno na kwa kutimia kwa mambo yaliyotabiriwa. Ilikuwa imetambulishwa dhahiri. Hapakuwepo haja kwake kufadhaika tena kuhusu hayo. Waona? Hapakuwepo haja kwa kuwazia cho chote juu yake kwa maana tayari ilikuwa wazi. Alikuwa tayari amefanya mambo haya. Aliisha kuthibitisha kwa inzi na viroboto ya kwamba alinena kisha vitu vikaumbika—ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ndani yake. Kwa hivyo hapa yuaenda kumuuliza Mungu la kufanya wakati mambo yanamkabili yeye. Waona? Lo, Jamani!

Natumaini hili linatuingia ndani, na tunaweza kuona mahali tulipo, mwaona? Si inakufanya ujisikie mkubwa hivi? Tukiwazia habari za Musa, tukizungumza kuhusu makosa yake, na kutazama yale yetu.

Hapa alikuwa an asimama pale, waona? Alijua ya kwamba Maandiko yalisema kwamba hiyo ilikuwa ndiyo saa na siku kwa hayo kutendeka, naye alijua ya kwamba Mungu alikuwa amekutana naye katika Nguzo ya Moto. Nayo ikashuka moja kwa moja mbele ya watu na kufanya hii miujiza na kila kitu alichosema, kilitendeka, hata kuumba vitu akifanya mambo ambaye ni Mungu tu angalifanya—akionyesha ya kwamba sauti yake ilikuwa Sauti ya Mungu. Na hapa hali ya mambo ikatukia kati ya watu aliokuwa akiwalea, akiwaongoza hata kwenye Nchi ya Ahadi, na huku anasimama akilia, “Nifanyeje?”

Huyo ni mwanadamu tu akitaka ku...kama Ndugu Roy Slaughter (naamini anaketi nje ya ule mlango pale) alivyoniambia wakati mmoja kuhusu mtu fulani akinifanyia jambo fulani, nami nikasema, “Vema, nilifanya hivi na sasa vile...”

Naye akasema, “Ndugu Branham, waache waegeme mabegani mwako, na kesho utawabeba.”

Na hivyo ndivyo wanadamu walivyo. Wanaegemea mebegani mwako leo, na kesho unawabeba. Hivyo ndivyo Musa alikuwa akifanya. Ilimbidi Mungu kumbeba baada ya kumchagua kuthibitisha kufanya hivyo! Nao hao watu iliwapasa kusema, “Musa, sema neno. Nilikuona ukifanya hivyo kule. Mungu

alikusikia kule. Nawe ndiwe mtu yule yule leo.” Amina. Mwaona? “Fanya hivyo!” Amina. Iлимпasa kujua hayo, bali hakujua. Vema.

Jinsi ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa. Tunaona ya kwamba—kwa hivyo yeye akasema. . . Hapana shaka Mungu alikuwa amechoka nayo. Hapana shaka Mungu alichoshwa nayo. Akasema, “Mbona unanililia Mimi? Je, Mimi tayari sijathibitisha utambulisho Wangu? Je, sijakwambia ya kwamba nilikutumia hiyo kazi. Sikukuambia uende ukafanye hili? Sikuahidi ya kwamba ningetenda haya, ya kwamba ningekuwa pamoja kinywa chako. Nami ningenena kupitia kwako nami ningefanya hivi nawe uonyeshe ishara na maajabu, sikuahidi hivyo? Je, Mimi sijaangamiza kabisa kila adui aliyekuzingira? Na ndiwe huyu hapa umesimama hapa sasa kwenye Bahari ya Samu ukitenda niliyokwambia kutenda na ungali unapiga makelele na kunililia Mimi. Je, uniamini Mimi? Je, huwezi kuona ya kwamba nilikutuma kufanya hivi?

Lo, huo si ubinadamu, jamani! Kwa hivyo, hapana budi ilimchosha kabisa. Naye akasema, “Unajua unaihitaji. Unajua kama utawapeleka hawa wana kule katika Nchi ya Ahadi. . . Hiyo ni kweli hasa. . . Umesongwa hapa pembeni. Hamna cho chote kingine unachoweza kufanya. Kwa hivyo, kuna haja. Sababu gani unanililia? Unataka nini Kwangu? Unaiitia nini? Je, sijaithibitishia watu? Sijaithibitisha kwako? Sijaiita? Si ni kulingana na Maandiko? Sikuahidi kuwapeleka watu hawa katika ile nchi? Sikukuita na kukuambia ya kwamba nitafanya hivyo? Sikukuita na kukwambia nimekutuma kufanya hivyo, na haikuwa wewe, ilikuwa Mimi? Nami nitashuka na nitakuwa pamoja na kinywa chako. Cho chote ulichosema, nilikithibitisha na kukishuhudia. Si nimefanya hivyo? Basi wakati jambo lo lote ndogo linapozuka, mbona unatenda kama mtoto? Inakupasa kuwa mtu mzima. Nena na watu! Amina. “Kisha mwendelee mbele.” Amina. Ndivyo hivyo “Usilie, nena!” Amina.

Jamani, napenda hilo. “Mbona unanililia? Nena tu na watu, kisha songeni mbele kwa shabaha yenu.” Cho chote kile, kama ni magonjwa, cho chote kile, kama ni kufufua wafu ama cho chote kile, nena! Nilithibitisha hayo. Nena na watu!”

Ni funzo jinsi gani! Ni funzo jinsi gani! Lo, jamani! Katika sehemu hii ya safari tunakosimama. Tazama tuliko sasa—naam, bwana!—katika Mvuto wa Tatu. Tazama, tuko papa hapo mlangoni wa kule kuja kwa Bwana.

Yeye alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya hiyo kazi walakini alikuwa akingojea BWANA ASEMA HIVI. Hapana shaka Mungu alichoshwa na hayo. Alisema, “Usilie tena; nena! Nilikutuma.”

Ee Mungu! Kile kanisa hili linachopaswa kuwa asubuhi ya leo! Mungu tayari amethibitisha kwa Nguzo ya Moto na ishara na maajabu—kila kitu kama tu ilivyokuwa katika siku za

Sodoma. Alisema zitajirudia. Ulimwengu ndio huu hapo katika hali yake, na taifa ni hili katika hali yake. Wanawake ndio hao hapa katika hali hiyo. Mtu yuko katika hali hiyo. Kanisa liko katika hali hiyo. Kila kitu kiko vile. Vitu vyote, zile ishara—visahani virukavyo angani na kila kitu angani na kila namna ya vitu vya ajabu na uvumi wa bahari, mawimbi ya baharini, watu wakivunjika mioyo kwa hofu, uoga, mashaka ya nyakati hizi, na dhiki ya mataifa, kanisa likianguka, na yule mwasi akiinuka ambaye hujiinua juu ya yote—yaitwayo Mungu, yeye aketiye katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake—lo, jamani! Naye amezuru taifa hili!

Na kanisa limeunda chama, nao wote wamekusanyika pamoja kama malaya wa yule kahaba, na kila kitu kimeingilia ukahaba. Ukahaba! Ni nini?—kuwaambia wanawake wanaweza kukata nywele zao, kuwaambia wanawake wanaweza kuvalia suruali fupi, kuwaambia wanaume wanaweza kufanya *hivi* na wafanye *vile* na mhubiri akisema, “fanya *hivi*,” na injili ya ujamaa na kadhalika. Hamwoni huko ni kufanya uzinzi na Neno la kweli la Mungu. Naye Mungu ametutumia Neno Lake la kweli lisilo la kidhehebu, bila uhusiano kwake, na kutupa ile Nguzo ya Moto, Roho Mtakatifu ambaye amekuwa pamoja nasi sasa kwa miaka thelathini, na kila kitu alichobashiri na kusema kilitendeka vile hasa alivyosema kingetendeka.

“Nena na watu; hebuni tusonge mbele.” Amina. Tuna shabaha fulani, hiyo ni Utukufu. Na tuuendee. Tunaelekea kwenye Nchi ya Ahadi. “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio.”

“Nena na watu. Je, sijathibitisha hayo. Si hata nimepigwa picha miongoni mwenu na kila kitu kinginecho, na kufanya kila kitu ambacho kingefanywa kuwathibitishia ya kwamba niko pamoja nanyi? Si magazeti hivi majuzi yaliandika hiyo makala, uliposema hapa mimbarani yale yangetendeka hapa miezi mitatu kabla hayajatendeka na kuthibitisha—hata sayansi inajua habari zake. Na kila kitu ambacho nimefanya, nanyi mngali mnangoja. Nena na watu na msonge mbele hata kwenye shabaha yenu.” Amina.

Je, Nathani hakumwambia Daudi—Nathani, yule nabii—wakati mmoja alipomwona Daudi yule mfalme mpakwa mafuta, alisema, “Haya, fanya yote yaliyomo moyoni mwako; Mungu yu pamoja nawe.” Kamwambia Daudi, “Haya, fanya yote yaliyomo moyoni mwako; Mungu yu pamoja nawe.”

Yoshua alikuwa ametiwa mafuta kuitwaa nchi kwa ajili ya Mungu na kwa watu wake. Siku ilikuwa fupi; alihitaji wakati zaidi kwa ajili ya ile kazi aliyokuwa na upako wake na kuagizwa kuitenda. Yoshua—mwanadamu. Aliishatiwa mafuta. Mungu alimwambia, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, nitakuwa pamoja nawe.” Amina. Hiyo nchi, nitawapa. Nataka uende

kule na kuwafagilia mbali Wamaleki na wengineo, Wafilisti na Waperezi na hao wote mbali mbali—wafagilie mbali. Mimi ni pamoja nawe. Hamna mtu atakayesimama mbele yako siku zote za maisha yako. Hamna mtu atakayekusumbua. Ingia mle.”

Naye Yoshua akachomoa upanga wake akasema, “Nifuateni” Naye akafika kule, na ndiye huyu hapa akipigana. Basi, ilikuwa nini? Akawashinda adui. Walikuwa vikundi vidogo hapa na vikundi vidogo pale. Usiku ulipofika wote wangekusanyika na kufanya kikosi kizima na kama jeshi kubwa kupigana naye, na jua lilikuwa likitua. Alihitaji nuru zaidi. Jua lilikuwa likitua! Hakupiga magoti na kusema, “Bwana Mungu, nitafanyeje?” Alinena! Alikuwa na haja naye akasema, “Wewe Jua, simama kimya!” Naye hakulia hata kidogo; aliamuru: “Wewe Jua, simama kimya; nina haja ya jambo hili. Mimi ni mtumishi wa Bwana, nimetiwa mafuta kwa ajili ya kazi hii, nami nina haja. Simama kimya na usiangaze, na wewe mwezi, simama mahali ulipo,” hata alipomaliza vile vita na kuangamiza kitu hicho chote.

Nalo jua likamtii. Hamna kulia, alilizungumzia jua. Kasema, “Wewe simama kimya. Wewe jua, ning’inia pale, nawe mwezi, kaa ulipo.” Yeye hakulia, “Bwana nifanye nini? Nipe nuru zaidi ya jua.” Alihitaji nuru ya jua, kwa hivyo akaliamrisha, nalo jua likamtii. Lo, jamani! Yeye aliliamuru jua lisimame kimya.

Samsoni, aliyetiwa mafuta, aliinuka, amechaguliwa na Mungu, akapewa karama ya nguvu na kuagizwa kuangamiza taifa la Wafilisti—aliagizwa, akazaliwa humu duniani, akatiwa mafuta na Mungu kuwaangamiza Wafilisti. Siku moja walimshika makondeni bila upanga wake, bila mkuki, na elfu moja ya hao Wafilisti wenye silaha wakamshambulia wakati mmoja. Je, yeye alianguka chini na kusema, “Ee Bwana, nangojea ono? Ee, Mungu, nifanyeje? Niambie sasa la kufanya.” Yeye alijua alikuwa na haja. Hakupata kitu ila maskini mfupa wa kale wa taya ya nyumbu naye akawapiga Wafilisti elfu moja. Amina! Yeye hakumlilia Mungu. Alitumia karama yake yenye upako. Alijua ya kwamba alikuwa ametumwa kwa ajili ya hiyo kazi. Alijua alizaliwa kwa ajili hiyo. Alijua alikuwa ametiwa mafuta kwa kipawa, naye akawapiga Wafilisti elfu moja. Yeye hakumlilia Mungu. Mungu alimchagua na kuthibitisha kwamba alikuwa hivyo kwa mambo mengine aliyokuwa amefanya, naye alikuwa mtumishi wa Mungu aliyethibitishwa, akatiwa mafuta kuwaangamiza Wafilisti, naye akafanya hivyo! Haidhuru hali ya mambo ilikuwaje, alifanya hivyo. Yeye hakuuliza neno. Hiyo ilikuwa kazi yake. Mungu alikuwa akitenda kupitia kwake. . . Akachukua ile taya ya nyumbu akaenda kuwapiga Wafilisti.

Jinsi. . .naam, pigo kwa kitu hicho juu ya hizo fuvu za kichwa upana wa ichi moja na nusu ya shaba zingaliuvunjavunja mfupa huo katika vipande milioni moja, na akawapiga elfu moja yao, na kuwaua na ingawa hivyo akasimama nacho

mkononi mwake. Hakuuliza maswali yo yote. Hakulia. Alinena. Akawashinda.

Lo, jamani! Twaa Wafilisti. “Naweza kuwatwaa Wafilisti, Bwana? Najua ulinituma kufanya hivyo Bwana. Naam, Bwana, najua ulinituma kuangamiza taifa hili la Wafilisti. Sasa hapa, elfu moja yao wamenizunguka. Sina kitu. Nifanyeje sasa, Bwana?” Lo, jamani! Hamna kitu kitakachomhangaisha. Ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo. Hamna kinachoweza kukudhuru. Lo, si hata jambo moja. Haleluiya!

Alichukua alichokuwa nacho na kuwapiga. Hiyo ni kweli. Adui alipomzingira na kusema, “Sasa tumemshika ndani ya kuta, tumempata sasa. Tumemshikia upande wa ndani huku akiwa na mwanamke. Sasa tumeufunga kabisa huu mlango mzuri na kila mahali, naye hawezi kutoka. Tumempata.”

Samson hakulia, “Ee Mungu, wamenizingira kila mahali kwa hili dhehebu. Nifanyeje? Nimejiunga pamoja nao. Nifanyeje?” Yeye hakufanya hivyo kamwe. Aliondoka tu, akang’oa hilo lango, akaliweka begani mwake na kuondoka nalo. Amina!

Yeye alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo. Aliitwa na Mungu—hawakumfungia ndani. Sivyo, kamwe! Alienda na hayo malango. Hakuomba juu yake. Hakumuuliza Mungu afanye hivyo au la. Alikuwa kazini mwake kabisa. Amina! Amina! Amina! Kazini mwake kabisa.

Mbona kunililia Mimi? Nena, na mwendelelee.” Amina. “Usilie, nena.” Aliisha koma kulalamika na kulialia kama mtoto sasa. Anapaswa kuwa mtu mzima kutosha kunena. Hiyo ni kweli. Alijua ya kwamba karama yake iliyotiwa mafuta ya nguvu ingeamiza Mfilisti ye yote aliyesimama mbele yake. Amina. Basi hatujui hivyo, mnaona. Sisi tungali watoto wenye chupa midomoni mwetu na... Alijua hivyo! Alijua ya kwamba Mungu alimwinua kwa kusudi hilo, na hamna kitu ambacho kingalisimama mbele zake siku zote za maisha yake. Hamna kitu ambacho kingemwangamiza. Yeye aliinuliwa kwa kusudi hilo kama Musa alivyokuwa—hamna kitu ambacho kingalimzuia. Sio Wamaleki ama cho chote kile kingemzuia. Yeye yumo njiani kwenda katika Nchi ya Ahadi. Samsoni alijua alikuwa njiani.

Yoshua alijua angeteka hiyo nchi. Yeye alikuwa amethibitishwa. Neno la Mungu lilihidi hivyo, naye Roho Mtakatifu alikuwa hapo akiithibitisha. Yeye alikuwa njiani kwa hivyo hamna kitu ambacho kingemzuia. La, bwana. Alikuwa kazini mwa Mungu. Hangalizuiwa na cho chote, kwa hivyo akayatwaa yale malango na kujitwika mabegani mwake—uzani wake ukiwa tani nne ama tano—akayachukua hata kilele cha mlima akaketi juu yake—hamna kitu kingemzuia. Alikuwa na kipawa Chenye upake kutoka kwa Mungu.

Haikumpasa kulia, “Bwana, nifanye nini sasa.” Alikuwa tayari amemtia mafuta kufanya hivyo. Hiyo ilikuwa BWANA ASEMA HIVI. “Waangamizwe!” Haleluiya! “Waangamize! Nimekuinua kwa kusudi hilo.” Amina.

“Nifanye nini, Bwana? Nitafanya nini hapa katika Bahari Shamu?”

Je, sikukuambia ya kwamba nilikupa mlima kama ishara papa hapa? Utarudi kwa huo mlima, utawapeleka hawa wana katika hiyo Nchi. Sikukuita kwa kusudi hilo? Kwa nini unafadhaika juu ya jambo jingine lo lote kukuzuia. Nena kisha uanze mwendo.” Amina na amina. “Nilikuitia kusudi hili.”

Daudi, alijua ya kwamba aliisha tiwa mafuta, naye alithibitishwa kwamba yuna shabaha nzuri. Yeye alijua ya kwamba alikuwa na shabaha mzuri. Daudi alikuwa mtiwa mafuta; alijua hivyo. Naye aliposimama mbele ya Goliathi, hakulia kamwe, “Ee, Mungu, Nifanye nini sasa? Lakini, lakini, lakini, najua ulivyotenda nyakati zilizopita; uliniwezesha kuua dubu, na ukaniwezesha kumuua simba, na huyu Goliathi hapa, je?” Yeye hakufanya hivyo; alinena tu. Alisemaje? “Utakuwa kama walivyokuwa.” Na niko... Alinena na akasonga mbele.

Hakuomba dua kamwe; hakusali hata kidogo. Alijua alikuwa mpakwa mafuta. Amina. Yeye alikuwa amepakwa mafuta na hilo pigo la kombeo lilithibitisha jambo lifaalo. Alikuwa na imani katika kutiwa mafuta kwake. Aliamini ya kwamba Mungu angeongoza hilo jiwe moja kwa moja hata katikati ya hiyo kofia ya chuma ambapo ndipo tu mahali pangepigwa. Alikuwa amesimama pale. Alijua alikuwa na shabaha nzuri. Amina. Alijua Mungu alikuwa amemfanya hivyo. Amina. Alijua aliisha muua simba. Alijua aliisha muua dubu, bali hiyo ilikuwa kwa mali ya baba yake wa duniani. Ndiyoo hii hapa mali ya Baba yake wa Mbinguni. Amina.

Hakujilaza chini, “Nifanyaje, Bwana?” Alinena akasema, “Utakuwa kama yule simba na yule dubu, haya, ndimi huyu naja.” Amina. Utukufu kwa Mungu! Naam, bwana.

Alinena kisha akasonga mbele kumkabili huyu Goliathi (lo, jamani!) bila kujali ukubwa. Alikuwa ni kijana tu, mwekundu, mwajua. Hakuwa mkubwa sana, hakuwa mwenye sura nzuri sana ukimtazama—kijitu cha mtu. Biblia ilisema alikuwa mwekundu. Basi, bila ukubwa wake, na wanaouita uweza wake wa kufanya hivyo...

Mwajua, Askofu alimwambia, kasema, “Sasa angalia hapa, mwanangu, mtu huyo ni mwanatheologia. Waona? Yeye ni mwanajeshi. Alizaliwa mwanajeshi naye amekuwa akipigana tangu utoto wake; nawe huwezi kujilinganisha naye.”

Nao ndugu zake wakasema, “Lo, mtukutu wee! Unakuja humu na kufanya jambo kama hilo; rudi nyumbani.” Hilo halikumhangaisha. Kwa nini?—alijua alikuwa ametiwa mafuta.

“Mungu aliyeiniokoa na yule simba, Mungu aliyeiniokoa na makucha ya huyo dubu, ataniokoa hata zaidi na yule Mfilisti. Ndimi huyu naja. Nakujia wewe kwa Jina la Bwana Mungu wa Israeli.” Amina

Hakuomba hata kupata ushindi—alikuwa tayari ameomba kutosha; Mungu alimwombesha kutosha kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Alikuwa amepakwa mafuta kwa ajili ya hiyo kazi. Iлимпasa kunena na kusonga mbele. Hayo tu ndiyo yalipaswa kufanywa. Kunena na kusonga mbele.

Lo, hivyo tu ndivyo ilivyokuwa. Yeye haku...kuhusu ndugu zake wa kidini, hao wadhihaki wakisimama pale, pia, mwajua. Lo, naam. Walisimama pale wakisema wakimdhihaki, na kumfanyia mzaha wakisema (ndugu zake, mwajua) na kumwambia... “Ah, ah, ah, mtukutu wee.” Hilo halikumtikiza hata kidogo. “Unataka kuwa tofauti na wengine, unataka kujionyesha tu.”

Kama hiyo ilikuwa kujionyesha, ingekuwa hivyo. Bali wao walitazamia tu upande wa akili. Daudi alijua mafuta ya upako yalikuwa juu yake. Haikuleta tofauti kwake. Yeye alisema, “Huyo Mfilisti atakuwa kama yule dubu na yule simba, kwa maana mimi hapa naja.” Alibashiri hayo kabla hayajatendeka. Alifanyaje?—aliva dubu; akaua simba. Akamwangusha simba chini. Kwa nini?—kwa kombeo, akatwaa kisu kisha huyo dubu—simba, alimuua simba kwa kisu. Hivyo ndivyo alivyomfanyia Goliathi. Alimwangusha kwa jiwe, kisha akauchomoa upanga wake, akakikata kichwa chake papo hapo mbele yao... Alitabiri nini kabla haijatendeka?—“Nawe utakuwa kama walivyo.” Kwa nini? Alinena neno ya kwamba itakuwa hivyo, ndiposa akasonga mbele kulifanya litimie. Amina. Lo, ndugu! Yeye alinena na akatawala hali ya mambo siku hiyo.

Kama kulikuweco na wakati ambapo mtu anapaswa kunena, ni sasa. (Nitamaliza tu katika dakika chache zifuatazo kama mnaweza tu kunistahimili kwa dakika chache tu. Nina mambo mengine yaliyoandikwa hapa, Maandiko machache ninayotaka kuyafikia).

Petro hakulia alipompata mtu aliyekuwa na imani ya kutosha kuponywa, ameketi katika mlango uitwao Mzuri. Hakupiga magoti na kuwa na maombi ya usiku kucha kisha ama maombi ya mchana kutwa, ama ombi refu sana na kusema, “Bwana, nakuomba, Wewe sasa, ya kwamba utamsaidia maskini mtu huyu kiwete. Naona ya kwamba yeye yuna imani. Najua ya kwamba yeye ni mwamini, nami nimemuuliza, naye amesema ana imani—angeamini niliyomwambia. Nilimwambia yale Wewe

uliyofanya, nami nafikiri tu sasa, Bwana... Je, waweza kunipa mimi BWANA ASEMA HIVI kwa ajili yake?"

Hasha, alijua ya kwamba alikuwa mtume mtiwa mafuta. Alijua ya kwamba Yesu Kristo alikuwa amemwagiza: "Waponye wagojwa, wafufue wafu, watakase wenye ukoma, watoe pepo; mmepata bure, toeni bure." Yeye akasema, Petro, nenda kafanye hivyo!" Haikumpasa kuomba hata apate ushindi, yeye alikuwa ameagizwa.

Je, alisemaje? Alisema, "Katika Jina la Yesu Kristo..." Yeye alitaja Jina la Yesu Kristo, naye huyo mtu akaketi tu pale. Akamshika mkono na kusema, "Simama kwa miguu yako!" Alimshikilia pale hata mifupa yake ya vifundo vya miguu ikapata nguvu, naye akaanza kutembea.

Kwani? Hakuwa na maombi ya usiku kucha. Hakumlilia Mungu kamwe. Yeye alijua yakini kutoka kwa kinywa cha Yesu Kristo alikuwa tayari ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hii. Yeye alinena na kumwinua juu kwa sababu alijua yeye alikuwa mtume mtiwa mafuta kwa kusudi hilo.

Watu walioketi kivulini mwake hawakusema kamwe, "Ee, njoo, Mtume Petro, ukatulilie na kutuombea kwa Mungu ombi la imani." La, la, hao hawakusema hivyo kamwe. Walijua alikuwa mpakwa mafuta na mtume wa Mungu aliyethibitishwa. Kwa hivyo wakasema, "Hebuni tukae kivulini mwake. Si lazima useme neno. Tunaajua; tunaamini." Uhai uliokuwa ndani yao... huyo mtume hangaliwafikia wote na wao wenyewe—wao ni sehemu yake.

Musa alisema, "Si mimi tu ninayeenda, sote twaenda. Sote tuna jambo la kufanya. Sote hatuna budi kupata upako." Nao wakamwona mtume huyo amesimama pale na kumwona akimponya yule mgojwa na kutenda mambo haya aliyotenda—walijua hangaliwafikia, kwa hivyo hao hawakusema, "Petro, njoo utuombe kisha ungoje sasa hata utakapopata BWANA ASEMA HIVI halafu uniambie" (mwona) "yale Bwana aliyosema." Walisema, "Laiti tungelililaza tu kwenye kivuli chake kwa sababu Mungu yule yule aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo yu ndani yake, na tumeona jambo lile lile likitendeka." Kwa hivyo akagusa upindo wa vasi la Yesu na kujilaza kivulini mwake na Yesu alikuwa katika mtu huyu. Kama kivuli hicho kikiwaangukia, wataponywa. Na Biblia ilisema kila mmoja wao aliponywa. Si maombi ya usiku kucha. Kusema, "Bwana, kama nikienda na kulala katika kivuli cha mtume huyu..." La, walijua. Nuru ilikuwa imewagusa. Mioyo yao ilikuwa imejaa, imani yao ilifunguliwa. Amina. Waliiamini na kuiona. Leso za Paulo—vile vile. (Sasa, tukimaliza).

Yesu hakulia walipomletea yule mvulana mwenda wazimu aliyekuwa na kifafa, akianguka motoni. Yeye hakusema kamwe, "Baba, Mimi ni Mwanao, nawe ulinituma huku kufanya *hivi*

na vile basi je, naweza kumponya mvulana huyu?" Yeye hakusema... Alisema, "Mtoke huyu, Shetani!" Yeye alinena kisha huyo mvulana akaponywa.

Alipokutana na yule Legioni mwenye pepo elfu mbili—si Yesu aliyelia; ni pepo waliolia. "Kama utatutoa, (jamani!) turuhusu tupate kuliingia lile kundi la nguruwe."

Yesu hakusema kamwe, "Sasa, Baba, naweza kutenda hili?" Yeye alisema, "Mtokeni," nao hao pepo wakapiga mbio. Bila shaka, Yeye alijua alikuwa Masihi.

Kaburini mwa Lazaro, (alikuwa amekufa kwa muda wa siku nne) wao walisema, "Kama ungalikuwa hapa, Bwana, hangalikufa."

Yeye akasema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima..." Si wapi, lini, ama vipi. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi." Amina. Yeye alijua alikuwa nani. Alijua alichokuwa. Alijua alikuwa Imanueli. Alijua alikuwa huo Ufufuo. Alijua alikuwa Uzima. Alijua ya kwamba katika Yeye mlikaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Aliwaona maskini watu hao pale na akaona ya kwamba yale Mungu aliyomwambia—aliyoambiwa afanye na ndiye huyo pale—akashuka akaenda kule.

Yeye hakusema kamwe, "Sasa ngoja, nitapiga magoti hapa nanyi nyote mpige magoti pia, tuombe." Alisema, "Mnaamini ninaweza kufanya hivi?" Amina. Naam. Bwana. Haikuwa Yeye; ni wao.

"Naam, Bwana, naamini ya kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni." Lo, jamani! Ndiye huyo hapa anathibitishwa. Jambo fulani halina budi kutendeka.

"Lazaro, njoo huku nje!" Akanena, kisha mtu aliyekufa akatoka nje. Si eti, je, ninaweza? Yeye alinena tu. Imani ilipotimilizwa, jambo hilo likatendeka.

Yeye hunena—alinena na vipofu wakapata kuona; viwete wakatembea; viziwi wakasikia; pepo wakalia kwa sauti kuu na kutoka; wafu wakafufuliwa—kila kitu. Kwa nini? Yeye hakuomba hata akapata ushindi; Yeye alikuwa Masihi mtiwa mafuta. Alikuwa yule Masihi. Alijua alikuwa hivyo. Alijua mahali pake. Alijua aliyotumwa kufanya. Alijua ya kwamba Baba aliisha mtambulisha kuwa Masihi kwa waamini; naye alipokutana na huyo mwamini mwenye imani, alinena tu Neno. Pepo wakatawanyika. Naam, bwana. Nena; usilie, nena! Amina.

Naye alijua haki Zake alizopewa na Mungu, bali sisi hatujui. Alijua alichokuwa; sisi hatujui.

Musa alikuwa amesahau. Samsoni alifahamu. Wengine walifahamu. Yoshua alifahamu. Musa akasahau. Ilimbidi Mungu kumkumbusha. Alisema, "Mbona unanililia Mimi? Nalikutuma kufanya hiyo kazi; nena! na uendelee kwa lengo lako.

Nalikuambia utakuja kwenye mlima huu; ukawachukue hao wana uwaongoze. Nena tu; sijali kitakachokuzuia, kiondoshe. Nimekupa mamlaka kufanya hivyo. Nalinena, ulinena inzi na chawa, na maumbile na vitu kama hivyo. Basi, mbona unipigie makelele? Mbona unakuja Kwangu, ukipiga makelele juu ya mambo haya? Nena tu uone ikitendeka, hivyo tu.” Lo, jamani! Lo, jinsi nipendavyo hilo.

Hapa Yesu...cho chote alichosema, Yeye alinena tu Neno, na ikawa hivyo. Mungu alikuwa amemthibitisha kabisa kuwa Mwanawe. “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. Msikieni Yeye.”

Mtazame. (Napenda hili) Jinsi alivyosimama kwa ujasiri na fahari mbele ya wapinzani wake. Amina. Alisema, “Livunjeni hili hekalu, nami nitamwomba Baba, nione atakavyofanya juu yake. Livunjeni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena. Si: *Natumainia; nitajaribu*—nitafanya hivyo! Kwa nini?—Maandiko yalisema hivyo. Maandiko yale yale yaliyosema ya kwamba Yeye angeufufua mwili Wake, yanatupa mamlaka, uweza. Amina! “Katika Jina langu watatoa pepo; watanena lugha mpya; wakishika nyoka ama wakinywa vitu vya kufisha; havitawadhuru kabisa. Wakiweka mikono yao juu ya wagojwa, watapata afya.

“Mbona unanililia? Nena na msonge mbele.” Lo, ujasiri—“Livunjeni hekalu hili, Nami nitalisimamisha tena.”

Lo, na kumbukeni sasa, (tunamaliza,) ilikuwa ni *Yeye* yule yule aliyesema katika Yohana 14:12: “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Sivyo? Ilikuwa ni yeye aliyesema hivyo. Ilikuwa Yesu katika Marko 11:24 aliyesema, “Ukiuambia huu mlima...” (si “ukiuombea huu mlima”) “. . . ukiuambia huu mlima ‘ng’oka,’ na usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba hayo usemayo yametukia, yatakuwa yako.” Sasa, kama ukisema tu kwa kubahatisha, haitatendeka, bali kama mna kitu ndani yako—ya kwamba umetiwa mafuta kwa kazi hiyo, na utajua kwamba ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, na utasema hivyo, haina budi kutendeka. “Mkikaa, . . .” Ni Yeye aliyesema hivi: “Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakae ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Lo, jamani! Jamani! Mnaona ninayomaanisha?

Kunradhi kwa hili jambo, bali limenijia mimi. Sina budi kulisema. Ilikuwa ni Yeye aliyesema ile siku kule mwituni, “Hujapata mnyama,” Kisha akawaumba kuchakulo watatu wakasimama pale mbele yetu. Ni nini? Kunena tu Neno, kusema watakuweko, na ndio hao pale, na pale na wakawa. Ilikuwa ni Yeye aliyefanya hivyo. Charlie, Rodney, ilikuwa *Ni Yeye* kule Kentucky. Nellie, Margie, na wengine wenu, ilikuwa *ni Yeye* Mungu yule yule aliyekuweko nyuma kule na kunena na Musa

akisema, “Mbona unanililia Mimi? Nena Neno.” Ilikuwa ni Yeye aliyewafanya waweko. Ndiye. Ni Yeye. Jamani!

Ilikuwa ni Yeye aliyenipa lile ono yapata mwaka mmoja uliopita lililosema tungeenda kule, na hizi Mihuri Saba na jinsi kungekuweco na ngurumo kubwa itakayonguruma, na itakuwa mfano wa piramidi. Kisha *Look*—lile gazeti liitwalo *Life* likainakili—inaning’inia ukutani pale. Ilikuwa *Ndiye* aliyesema hivyo.

Ilikuwa ni Yeye usiku huo nilipokuwa nikitembea barabarani nikaona ile nyoka yenye sumu sana iitwayo mamba ikiwa karibu kumuuma ndugu yangu. Yeye akasema, “Umepewa nguvu za kumfunga ama wengine wote.”

Ilikuwa ni Yeye aliyemwambia huyo maskini mke wangu anayeketi kule nyuma—ilikuwa Ndiye ile asubuhi aliyeniamsha chumbani na nikuketi pembeni akisema, “Usiogope kufanya cho chote ama kwenda po pote ama kusema cho chote, kwa maana uwepo unaodumu daima wa Yesu Kristo uko pamoja nawe po pote uendako.”

Ilikuwa ni Yeye kule juu katika Magenge Marefu ya Sabino yapata miezi mitatu iliyopita nilipokuwa nikiomba, nikishangaa itakuwaje, nami nilipokuwa nimesimama pale upanga ukaanguka mkononi mwangu, kisha kasema, “Huu ni Upanga wa yule Mfalme.” Ilikuna ni Yeye.

Ilikuwa ni Yeye aliyeniambia mimi, “Kama nilivyokuwa na Musa, ndivyo nitakavyokutuma wewe.”

Ilikuwa ni Yeye aliyeniambia miaka thelathini iliyopita kule ng’ambo mtoni kama mvulana mdogo, nimesimama mle kama mhubiri kijana mtoni miaka thelathini iliyopita—nimesimama mle wakati ile Nuru na Nguzo ya Moto ile ile iliposhuka kutoka mbinguni na kusimama kule na kasema, “Kama nilivyomtuma Yohana Mbatizaji kukutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia kule kuja kwa pili”—ulimwenguni kote. Ingewezekanaje wakati mchungaji wangu mwenyewe aliicheka na kuifanyia mzaha? Bali ilitendeka vivyo hivyo hasa. Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni Yeye aliyesema hivyo. Naam, bwana!

Lo, jinsi ilikuwa ni Yeye aliyesema katika unabii, “Itatimia.” Ndiye aliyesema, “Kama mmoja miongoni mwenu anatoa unabii ama kuona ono na kulinena, nalo linatimia, basi kumbukeni huyo siye, ni Mimi. Mimi niko pamoja naye.” Lo jamani! Ningeendelea kusema, Ndiye, Ndiye, Ndiye.

Ndiye aliyeshuka . . . Nilipowaambia ya kwamba kulikuweco Nguzo ya Moto kule mtoni, nao hawangeamini. Ilikuwa ni Yeye kule kati . . . pamoja na huyo Mhubiri Mbatisti mbele ya watu elfu thelathini usiku huo katika Jumba kubwa mno la Michezo la Sam Houston wakati yule Malaika wa Bwana alipigwa picha amesimama pale. Ilikuwa ni Yeye yeye yule jana, leo na

hata milele. Ilikuwa *ni Yeye* aliyetabiri ni wapi mambo haya yangekuwa. *Ni Yeye* aliyesema haya. *Ni Yeye* aliyefanya mambo haya. Ni yeye yule jana, leo na hata milele. Ametenda kila kitu jinsi hasa alivyosema atatenda. Amina.

Kwanini ningoje? Mungu tayari amethibitisha Neno. Ni Kweli. Tuanze safari. Tushike njia ya Bwana, tukiweka kando mashaka yote, dhambi zote. Tuisafishe nyumba; tuisugue sana. Kama lilivyosema ono la Junior Jackson, hamna kilichobakia ila taa—ama doto yake, (iwapo anaketi hapa). Hamna kilichosalia ila taa, nazo zilizungushiwa milia ya dhahabu—katika doto aliyonisimulia mimi majuzi usiku. Jamani!

Ndugu Collins, usijali kuhusu yule samaki. Alikuwa mweupe; haukujua kamwe la kumfanyia. Weka kando cho chote kilicho kinyume chake. Kumbukeni hii ni Kweli haijalishi inaonekana ya mwenda wazimu vipi, kila kitu wakati mwingine. . . Endlea mbele tu pamoja nayo.

Ni Roho Mtakatifu, Mungu yule yule aliyemfufua Yesu Kristo kutoka katika wafu. Ndiye yule yule anayeweza kunena vitu hivi hata vikawa, yeye yule aliyeishi katika siku za Musa ni yeye yule leo. Mwito Wake katika hizi siku za mwisho, Yeye tayari amethibitisha, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu ajapo.” Ametenda. . . Kuna Sodoma kule. Kuna Billy Graham na Oral Roberts kule nje, na kanisa linapiga hatua kwa ishara zile zile alizoahidi mahali pote pawili, na ziko pale. Ndiye alisema hivyo. Ee, Mungu, nipe ujasiri, ndio ombi langu. Nisaidie, Ee Bwana Mungu.

Sina budi kuachia hapa. Tumachelewa.

Mbona unalililia Mimi? Mbona unanililia Mimi na tayari nimethibitisha kuwa pamoja nawe? Je, sijawaponya wagojwa wenu,” Yeye angesema? Sijawaambieni mambo ambayo yalitendeka vivyo hivyo hasa? Mchungaji wenu hawezi kufanya hivyo. Hawezi. Yeye ni mwanadamu. “Ni Mimi, Bwana,” ndivyo angesema. “Ni mimi niliyefanya hivyo. Mimi Ndimi ninayemwambia mambo haya. Si yeye. Ni Sauti Yangu. Mimi ndimi ninayewafufua wafu wenu wanapoanguka chini. Mimi ndimi ninayewaponya wagonjwa. Mimi ninayetabiri mambo haya. Mimi ndiye ninayeokoa. Mimi ndimi ninayetoa ahadi.”

Mungu, nipe ujasiri kuutwaa huo Upanga wa Neno ulionikabidhi mkononi mwangu yapata miaka thelathini na mitatu iliyopita na kuushika na kupiga hatua mbele hata katika ule Mvuto wa Tatu ndilo ombi langu. Hebuni na tuinamishe vichwa vyetu.

Baba wa Mbinguni, wakati unakwisha, bali Neno linakuwa lenye thamani. Kama tunavyouona, Bwana, wakati baada ya wakati, uwepo unaodumu wa Kristo daima hukutana nasi. Jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya wema Wako, jinsi

ulivyotuhifadhi na kutubariki; jinsi tunavyokushukuru kwa ajili yake.

Ninapozishika hizi lesi mkononi mwangu, Bwana—ni watu walio na imani wanaoamini hili. Na kila pepo, kila ugonjwa uwaondokee watu hawa. Namwamuru kila pepo hapa aliye mchafu na asiye wa Mungu, kila pepo wa magonjwa, magonjwa yote na mateso—sisi hatujilazi katika kivuli cha mwanadamu, ambayo ingekuwa sawa, bali tuko kwenye kivuli cha Injili—Injili iliyothibitishwa.

Huku ile Nguzo kuu ya Moto inapoenenda huku na huko humu jengoni, ile ile ambayo Mungu alitazama, kupitia, nayo Bahari ya Shamu ikaachana, nao Israeli wakapita. Bali sasa, Yeye anapotazama, imenyunyiziwa Damu ya Mwanawe Pekee—ambapo rehema na neema... Na tuwe watiifu; na leo tuache kusema—kulilia. Hebu na tutambue ya kwamba umetuitia jukumu hii. Huu ndio wakati ufaao. Nanena katika Jina la Yesu Kristo. Hebu kila ugonjwa uondoke mahali hapa.

Na kila mwanamume na mwanamke aliitiaye Jina la Yesu Kristo aweke maisha yake wakfu upya leo. Nayaweka yangu wakfu, Bwana, juu ya madhabahu ya maombi. Najilaza chini na kujionea haya na kuelekeza kichwa changu ardhini ambako ulinitoa.

Bwana Mungu, naona haya kwa ajili ya unyonge wangu na kutokuamini. Nisamehe, kwayo hayo Bwana; nipe ujasiri. Tupe sote ujasiri. Najisikia kama Musa—sote tuko njiani tukitoka. Hatutaki kumwacha mtu hata mmoja. Tunataka kuchukua kila mmoja, Bwana. Wote ni Wako. Nawadai kwa ajili Yako. Wabariki watu hawa leo, Bwana; tujalie. Nibariki pamoja nao, Baba, nalo Jina Lako litasifiwa; Utukufu Wako utakuwa Wako. Tupe imani ya Milele, Bwana, tunapojiweka wakfu Kwako sasa. Mimi, juu ya hii Biblia, juu ya jukwaa hii, nakupa Wewe maisha yangu, Bwana. Ninategemea kila ahadi uliyotoa. Najua ya kwamba zitathibitishwa. Najua ni Kweli. Nipe ujasiri kunena maneno haya. Nipe ujasiri, Bwana. Niongoze kwa yale nitakayofanya na kusema. Najitolea Kwako pamoja na kanisa hili, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

“Yesu kwa imani
Nakutumaini,
Peke Yako!
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni Wako Kabisa
Tangu leo.

Basi, hebuni tusimame kimya sana tunapouvumisha.

[Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanaugugumiza huo wimbo—Mh],

Hebuni tumwinulia mikono yetu. Tujiweke wakfu kwa Mungu sasa.

“...Nisikie sasa
Ondoa mashaka yangu yote,
Ni Wako kabisa
Tangu leo!”

[Kusanyiko linakariri ombi hili nyuma ya Ndugu Branham—Mh.]

Naam, sote pamoja huku mikono yetu imeinuliwa:- Bwana Yesu, sasa ninajitoa Kwako. Maisha ya utumishi kwa usafi zaidi, imani zaidi, nakulilia, nipate kuwa mtumishi anayekubalika zaidi katika maisha yangu yajayo kuliko nilivyokuwa katika maisha yaliyopita. Nisamehe kutokuamini kwangu na uturudishie sisi imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Najitolea mwenyewe Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Tunapoinamisha vichwa vyetu...

Nipe Nguvu pia
Za kusaikia
Moyo wangu;
Ulikufa Wewe
Wokofu nipewe
Nakupenda Wewe
Bwana Wangu.

Tunapoviinamisha vichwa vyetu sasa: Mnajisikia kama huu ujumbe wa asubuhi umewafaidi kitu? Umewapa ujasiri? Mkiweza, mwinulieni Mungu mikono yenu mkisema, “Mungu, nakushukuru.” Nimeinua mikono yangu yote miwili kwa sababu najisikia kufanya hivyo kwa kuwa umenisaidia; umenipa ujasiri.

Baadhi ya mambo niliyosema, sikufikiria ningeyasema, bali yamekwisha kusemwa. Ni karipio kwangu mimi. Nilijikuta mwenyewe nikiwa katika njia sikufikiri nilikuwa hivyo, bali nalijiona mwenyewe nina hatia ya kulia wakati wote badala ya kunena. Mungu, nisaidie tangu wakati huu nipate kuwa mtumishi aliyejiweka wakfu. Sijiombei tu mimi pekee, nawaombea ninyi, pia, ya kwamba sote pamoja kama Mwili wa Kristo, tulioitwa tuko ulimwenguni, tukijitayarisha kuingia kwenye Nchi ya Ahadi, ya kwamba Mungu atanipa ujasiri kunena jinsi—kuifanya njia wazi kusudi msikose kuzifuatilia hizo nyayo. Nitawaambieni kwa neema ya Mungu. Nitazifuata nyayo Zake zilizojaa damu Yake Yeye aliyeenda mbele yetu, kisha...

“Msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba,
Hata mauti yatakaponiweka huru.
Kisha nitaenda nyumbani kuva taji,
Kuna taji kwa ajili yangu.”

Tunakupa hili Wewe, Baba—kuwekwa wakfu kwetu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

Tunamshukuru Bwana kwa hili—ishi maisha yaliyowekwa wakfu. Jitoleeni—kwa wema, unyenyekevu, enendeni katika Roho, enendeni, neneni, vaeni kama Wakristo, wanyenyekevu na wazuri, msikose hili sasa. Sauti ya Mungu hunena kupitia kwa Neno—hunena kupitia kwa karama. Karama moja inapokuja, nyingine huitangaza. Karama nyingine inakuja na kuonyesha jambo lilo hilo. Mwaona! Hilo linalingana kabisa na Neno na wakati huu pia. Mungu yu pamoja nasi. Jinsi tunavyomshukuru kwa ajili yake. Naam, huku vichwa vyetu vimeinamishwa—kama dada yetu angetupa tuni juu ya . . .

“Peleka Jina la Yesu
Po pote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Fanyeni hivyo tu, semeni Neno. Semeni Jina Lake. Hebuni tuimba sasa tunapopumukana:

“Peleka Jina la Yesu
Po pote uendako
Litafurahisha moyo
Peleka uendako.
Dhamani . . .”

Basi, hebu tusalimianeni kwa mikono na kusema, nitakuombea, ndugu; nawe niombee.

“Ni Jina Lake Yesu;
Dhamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.”

Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu tuimbe aya hii inayofuata.

“Peleka Jina la Yesu
Ndilo silaha Yako
Utakapojaribiwa
Lilia Jina hilo.
Dhamani na tamu
Ni jina lake Yesu
Dhamani na tamu
Ni jina lake Yesu.”

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa pamoja na mioyo yetu, tukitambua ya kwamba Yesu alisema, “Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.”

Tukijua ya kwamba sisi, kwa neema ya Mungu tunao ndani ya mioyo yetu, tukijitakasa Kwake asubuhi ya leo kusudi maisha yetu yapate kubadilika tangu leo na kuendelea, tupate kuwa na mawazo mema. Tutajaribu kuishi vizuri sana na kuwa wanyenyekevu pia tukiamini yale tunayomwomba Mungu,

Mungu atampa kila mmoja. Nasi hatutanena maovu sisi kwa sisi ama dhidi ya mtu ye yote. Tutawaomba adui zetu na kuwapenda; tuwafanyie mema wanaotufanyia mabaya. Mungu ndiye Hakimu wa asiye na makosa na aliye na makosa. Lakini kwa msimamo huu na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nitamuuliza rafiki yetu mwema Ndugu Lee Vayle, kama atafunga mkutano kwa maombi. Ndugu Vayle.

[Ndugu Vayle anaomba—Mh.]



MBONA UNALIALIA? NENA! SWA63-0714M

(Why Cry? Speak!)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Julai 14, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2011 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org